



**SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR
WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA AMALI**

HOTUBA YA WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA AMALI

MHE. LELA MUHAMED MUSSA (MBM)

**KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA
KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027**

MEI, 2026

YALIYOMO

| | |
|---|----|
| YALIYOMO..... | i |
| UTANGULIZI | 1 |
| VIPAUMBELE VYA WIZARA NA TAASISI ZILIZO CHINI YAKE KWA MWAKA 2025/2026 | 5 |
| UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA MSINGI YA WIZARA | 7 |
| MAPATO..... | 7 |
| UTEKELEZAJI WA PROGRAMU KUU NA NDOGO KWA MWAKA 2025/2026..... | 8 |
| MUUNDO WA PROGRAMU | 8 |
| PROGRAMU YA KWANZA: ELIMU YA MAANDALIZI NA MSINGI | 10 |
| PROGRAMU YA PILI: ELIMU YA SEKONDARI..... | 13 |
| PROGRAMU YA TATU: ELIMU YA JUU..... | 16 |
| Programu ndogo ya Mafunzo ya Ualimu | 17 |
| Huduma ya Elimu ya Juu, Ushauri na Utafiti | 20 |
| Huduma ya Sayansi na Teknolojia | 23 |
| Huduma ya Teknolojia – IIT Madras | 25 |
| Huduma ya Mikopo ya Elimu ya Juu | 26 |
| Huduma ya Uratibu wa Elimu ya Juu | 28 |
| PROGRAMU YA NNE: ELIMU MBADALA NA MAFUNZO YA AMALI..... | 30 |
| Programu ndogo ya Elimu Mbadala na Watu Wazima | 31 |
| Programu ndogo ya Mafunzo ya Amali | 32 |
| PROGRAMU YA TANO: UBORA WA ELIMU | 36 |
| Huduma ya Mitaala na Vifaa vya Kufundishia | 36 |
| Huduma ya Upimaji na Tathmini ya Elimu..... | 39 |
| Huduma ya Ukaguzi wa Elimu | 42 |

| | |
|--|----|
| Huduma za Maktaba | 44 |
| Huduma ya Baraza la Elimu | 46 |
| Programu ndogo ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano katika Elimu | 48 |
| Programu ndogo ya Elimu Mjumuisho na Stadi za Maisha .. | 50 |
| Programu ndogo ya Michezo na Utamaduni | 52 |
| PROGRAMU YA SITA: UTAWALA NA UONGOZI | 54 |
| Programu ndogo ya Uongozi kwa Ujumla | 55 |
| Programu ndogo ya Mipango, Sera na Utafiti | 57 |
| Programu ndogo ya Uratibu shughuli za elimu Pemba..... | 59 |
| UTEKELEZAJI WA VIPAUMBELE KWA MUJIBU WA MPANGO MKAKATI WA WIZARA NA TAASISI KWA MWAKA 2025/2026. . | 61 |
| MWELEKEO WA UTEKELEZAJI WA VIPAUMBELE VYA MATUMIZI KWA WIZARA NA TAASISI ZINAZOSIMAMIWA NA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027. | 63 |
| MPANGO WA UTEKELEZAJI KWA MWAKA 2026/2027 KATIKA MFUMO WA PROGRAMU..... | 67 |
| PROGRAMU YA KWANZA: ELIMU YA MAANDALIZI NA MSINGI | 67 |
| PROGRAMU YA PILI: ELIMU YA SEKONDARI..... | 69 |
| PROGRAMU YA TATU: ELIMU YA JUU..... | 70 |
| Programu ndogo ya Mafunzo ya Ualimu | 70 |
| Huduma ya Elimu ya Juu, Ushauri na Utafiti | 71 |
| Huduma ya Sayansi na Teknolojia | 72 |
| Huduma ya Teknolojia IIT Madras | 73 |
| Huduma ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu | 74 |
| Huduma ya Uratibu wa Elimu ya Juu | 75 |
| PROGRAMU YA NNE: ELIMU MBADALA NA MAFUNZO YA AMALI..... | 75 |

| | |
|--|----|
| Programu ndogo ya Elimu Mbadala na Watu Wazima | 75 |
| Programu ndogo ya Mafunzo ya Amali | 76 |
| PROGRAMU YA TANO: UBORA WA ELIMU | 77 |
| Huduma ya Mitaala na Vifaa vya Kufundishia | 78 |
| Huduma ya Upimaji na Tathmini ya Elimu | 78 |
| Huduma ya Ukaguzi wa Elimu | 79 |
| Huduma za Maktaba | 80 |
| Huduma ya Baraza la Elimu | 81 |
| Programu ndogo ya Elimu Mjumuisho na Stadi za Maisha .. | 81 |
| Programu ndogo ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) | 82 |
| Programu ndogo ya Michezo na Utamaduni | 83 |
| PROGRAMU YA SITA: UTAWALA NA UONGOZI | 85 |
| Programu ndogo ya Uongozi kiujumla | 85 |
| Programu ndogo ya Uratibu wa Shughuli za Mipango, Sera na Utafiti | 86 |
| Programu ndogo ya kuratibu shughuli za Elimu Pemba | 87 |
| MAKADIRIO YA MAPATO | 87 |
| JUMLA YA GHARAMA ZA WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA AMALI | 87 |
| SHUKURANI | 88 |
| KIAMBATISHO | 90 |

HOTUBA YA WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA AMALI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027

UTANGULIZI

- 1. Mheshimiwa Spika**, naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema na Mwenye Kurehemu, kwa kutujaalia neema ya uhai na afya njema na kutuwezesha kukutana katika Baraza hili Tukufu kwa ajili ya kuwasilisha Hutuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha kwa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa mwaka wa fedha 2026/2027.
- 2. Mheshimiwa Spika**, naomba kutoa hoja kwamba Baraza lako Tukufu likae kwa madhumuni ya kupokea na kujadili taarifa ya utekelezaji ya mwaka 2025/2026 na hatimae kuidhinisha Makadirio ya Mapata na Matumizi ya Fedha kwa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa mwaka wa fedha 2026/2027.
- 3. Mheshimiwa Spika**, napenda kutumia fursa hii kutoa pongezi za dhati kwa viongozi wetu wakuu, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mheshimiwa, Dkt. Hussein Ali Mwinyi, kwa Uongozi wao imara na wenye maono katika kusimamia rasilimali za umma na kuendelea kuipa Sekta ya Elimu nafasi ya pekee katika ajenda ya maendeleo ya nchi. Chini

ya uongozi wao, Serikali imeendelea kuimarisha upatikanaji wa elimu na kuweka msingi mzuri wa kuandaa wataalamu na nguvu kazi yenye ujuzi kwa maendeleo ya Taifa letu. Tunamuomba Mwenyezi Mungu aendeleo kuwajaalia afya njema, hekima na busara katika kuwatumikia wananchi. Aidha, tunatoa pongezi na shukurani za dhati kwa Makamu wa Pili wa Rais, Mheshimiwa Hemed Suleiman Abdulla, kwa namna anavyoendelea kumsaidia Mheshimiwa Rais kwa uaminifu na weledi katika uongozi wa nchi yetu. Hakika, mchango wake ni muhimu katika kuimarisha utekelezaji wa majukumu ya Serikali na kufanikisha azma ya kuijenga Zanzibar yenye maendeleo.

4. **Mheshimiwa Spika**, Kwa namna ya kipekee, napenda kutumia fursa hii kumshukuru kwa dhati Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dkt. Hussein Ali Mwinyi, kwa kuendelea kuniamini na kunitua tena kushika dhamana ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali. Uteuzi huu ni heshima kubwa kwangu na naupokea kwa unyenyekevu mkubwa, nikitambua uzito wa dhamana hiyo pamoja na matarajio makubwa ya wananchi na Serikali kwa sekta ya elimu. Imani aliyonionesha inanipa nguvu mpya ya kuendelea kuitumikia Taifa kwa uadilifu, weledi na kujituma zaidi katika kusimamia utekelezaji wa majukumu ya Wizara, kwa lengo la kuimarisha sekta ya elimu na kuchangia maendeleo ya Zanzibar.

- 5. Mheshimiwa Spika**, kwa unyenyekevu mkubwa, napenda kutoa shukurani zangu kwako wewe binafsi pamoja na Mheshimiwa Naibu Spika na Mheshimiwa Mwenyekiti wa Baraza la Wawakilishi kwa uongozi wenu mzuri katika kusimamia na kuratibu shughuli za Baraza hili Tukufu. Uongozi wenu umewezesha kuendelezwa kwa mijadala yenye tija katika kuisimamia Serikali na kuchangia ustawi wa wananchi katika nyanja mbalimbali za kiuchumi, kisiasa na kijamii. Kwa hakika, mchango wenu katika kuimarisha utendaji wa Baraza hili ni wa kutambuliwa na kupongezwa. Namuomba Mwenyezi Mungu awazidishie hekima, busara na afya njema katika kuendelea kuliongoza Baraza hili kwa maslahi mapana ya Taifa letu. Aidha, namshukuru Katibu wa Baraza la Wawakilishi pamoja na watumishi wote wa Baraza hili kwa utekelezaji mzuri wa majukumu yao na kwa kuwezesha shughuli za Baraza kutekelezwa kwa ufanisi mkubwa.

- 6. Mheshimiwa Spika**, aidha, napenda kutoa pongezi za dhati kwa Kamati ya Ustawi wa Jamii ya Baraza la Wawakilishi, chini ya uongozi wa Mwenyekiti wake, Mheshimiwa Hussein Ibrahim Makungu, kwa kazi nzuri wanayoifanya katika kufuatilia, kushauri na kusimamia utekelezaji wa masuala yanayohusu ustawi wa jamii, ikiwemo sekta ya elimu. Bila shaka, ushirikiano, maoni na ushauri wa Kamati hii umekuwa na mchango muhimu katika utekelezaji wa majukumu ya Wizara na kuimarisha maendeleo ya elimu nchini. Vilevile, napenda kuzishukuru Kamati nyengine zote za Baraza la Wawakilishi kwa mchango wao katika

kuisimamia Serikali, kutoa ushauri na kuhakikisha shughuli za maendeleo zinatekelezwa kwa ufanisi. Namuomba Mwenyezi Mungu aendelee kuziongoza Kamati hizi na kuwajaalia wajumbe wake hekima, afya njema na nguvu katika kutekeleza majukumu yao.

- 7. Mheshimiwa Spika,** Kwa namna ya pekee, napenda kuchukua fursa hii kumshukuru kwa dhati Mheshimiwa Ali Abdulghulam Hussein aliekuwa Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, Mheshimiwa Khadija Salum Ali, Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali kwa ushirikiano mkubwa walionipatia katika utekelezaji wa majukumu ya Wizara. Aidha, nawapongeza na kuwashukuru watendaji wote wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, wakiongozwa na Katibu Mkuu Ndugu Khamis Abdulla Said, Naibu Katibu Mkuu Taaluma Dkt. Mwanakhamis Adam Ameir na Naibu Katibu Mkuu Utawala Ndugu Amos John Henock, Ndugu Khalid Masoud Wazir aliekuwa Naibu Katibu Mkuu Utawala, Afisa Mdhamini Ndugu Mohammed Nassour Salim, Wakurugenzi, Wakuu wa Vitengo, Wenyeviti na Wajumbe wa Bodi mbalimbali za Elimu, Maafisa wa ngazi zote za Wizara, Walimu pamoja na Kamati za Skuli kwa ushirikiano, bidii na uwajibikaji wao katika kutekeleza majukumu ya Wizara. Mafanikio tunayoyaona katika sekta ya elimu ni matokeo ya juhudi za pamoja, nidhamu ya kazi na kujitolea kwa watumishi hawa katika kuwatumikia wananchi. Vilevile, napenda kutoa shukurani kwa wazazi, wanafunzi na wadau wote wa elimu wa ndani na nje ya nchi kwa kuendelea kushirikiana na Serikali katika utoaji

na uimarishaji wa huduma za elimu nchini. Nawaomba tuendelee kudumisha ushirikiano na mshikamano huu ili kwa pamoja tuweze kusukuma mbele mageuzi ya elimu kwa maendeleo ya Zanzibar.

8. **Mheshimiwa Spika**, mwisho nawashukuru sana watendaji wa Ofisi ya Rais Fedha na Mipango, Taasisi ya Afisi ya Rais Ufuatiliaji na Usimamizi wa Utendanji Serikalini (PDB), Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mdhambi na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, Mkaguzi Mkuu wa Ndani, Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu wa Uchumi Zanzibar (ZAECA), Ofisi ya Mufti Mkuu wa Zanzibar, Washirika wa Maendeleo, Asasi za Kiraia, Sekta binafsi pamoja na wananchi wote kwa mchango wao katika kufanikisha utekelezaji wa mipango ya elimu. Ushirikiano huu umeendelea kuwa msingi muhimu wa kuimarisha huduma za elimu na tunatarajia utaendelea kuimarika katika mwaka wa fedha 2026/2027.

VIPAUMBELE VYA WIZARA NA TAASISI ZILIZO CHINI YAKE KWA MWAKA 2025/2026

9. **Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka wa fedha 2025/2026, Wizara pamoja na Taasisi zake ilitekeleza kazi zake kupitia Vipaumbele Vikuu vifuatavyo:
 - i) Kuhamasisha jamii katika uandikishaji wa watoto skuli katika umri sahihi, kutoa mashirikiano katika usimamizi wa nidhamu za wanafunzi pamoja na ufuatiliaji wa Maendeleo yao ya skuli.

- ii) Kuimarisha miundombinu ya elimu kwa kuongeza idadi ya madarasa kupitia ujenzi wa skuli 20 za Maandalizi za chini, Skuli 21 za Msingi zinazojumuisha Skuli 16 za ghorofa na skuli 17 za Sekondari, kati ya hizo 12 za ghorofa. Aidha, Wizara imepanga kujenga skuli tatu za Elimu Mjumuisho katika Mkoa wa Kaskazini Unguja, Mjini Magharibi na Mkoa wa Kaskazini Pemba.
- iii) Kufanya ukarabati wa madarasa 900 na kukamilisha madarasa 300 yaliyoanzishwa kwa nguvu za wananchi.
- iv) Kuimarisha mazingira ya kujifunzia na kufundishia kwa kujenga vyoo 700 katika skuli za Maandalizi, Msingi na Sekondari, Dakhalia 09, nyumba 10 za walimu, kuziimarisha dakhalia kwa kuziwekea miundombinu ya gesi, kuweka mifumo ya umeme wa jua katika skuli 35 za ghorofa pamoja na kununua samani za skuli zenye ubora.
- v) Kuimarisha Miundombinu ya Ofisi kwa kutanua jengo la Makao Makuu ya Wizara, jengo la Ofisi ya Baraza la Mitihani na Kituo cha Kuchapisha Mitihani, Ofisi ya Mamlaka ya Mafunzo ya Amali, ujenzi wa chuo cha ubaharia (SUZA), utanuzi wa chuo cha Karume, kujenga Maktaba kuu mpya ya kisasa na Ujenzi wa Chuo cha IIT Madras.
- vi) Kuimarisha matumizi ya teknolojia katika kujifunzia na kufundishia kwa kuzipatia Skuli vifaa vya TEHAMA vikiwemo Smart Screen 25, Kompyuta za Mezani 2,000, Mbao za Mahudhurio za Kidijitali (School Digital-Attendance Board), Laptop 3,000, kuweka vifaa vya

TEHAMA kwa ajili ya Maktaba Mtandao katika skuli 33 za Unguja na Pemba.

- vii) Kuendelea kutekeleza mtaala mpya wa umahiri kwa elimu ya Maandalizi, Msingi na Sekondari kwa kuwapatia walimu mafunzo ya namna bora ya kutekeleza mtaala wa umahiri, kuendelea kuandaa na kuchapisha vitabu vya kiada na viongozi vya Mwalimu ili kusaidia kutekeleza mtaala huu.
- viii) Kuimarisha Mafunzo ya Ufundi na Amali kwa kujenga vyuo vitano vya Mafunzo ya Amali na karakana kwa ajili ya mafunzo ya Amali na Ufundi katika skuli 25 za Sekondari pamoja na kuzipatia vifaa.
- ix) Kuimarisha Michezo na Utamaduni kwa kujenga Sport Academy na viwanja viwili vya michezo vya kisasa katika skuli zenye michepuo ya michezo na kuzipatia skuli vifaa.
- x) Kuimarisha Elimu ya Juu kwa kuongeza fursa ya upatikanaji wa mikopo kwa wanafunzi wa Elimu ya Juu Zanzibar kuanzia ngazi ya Diploma.

UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA MSINGI YA WIZARA

- 10. Mheshimiwa Spika**, sasa naomba kuwasilisha utekelezaji wa Majukumu ya Msingi ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa mwaka wa 2025/2026 kama ifuatavyo: -

MAPATO

- 11. Mheshimiwa Spika**, Wizara imeendelea kukusanya mapato kupitia usajili wa Skuli za binafsi, malipo ya leseni za walimu,

ada za usajili wa skuli, ada za kiingilio kwa wanafunzi wanaojiunga na kidato cha sita na usajili wa wanafunzi wa skuli binafsi wanaofanya mitihani ya Taifa na usajili wa vituo vya kufanyia mitihani. Hadi kufikia Aprili 2026, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali imekusanya jumla ya **Tsh. 603,365,096** kati ya **Tsh. 3,200,200,000** zilizopangwa kukusanywa. Hii ni sawa ya asilimia 18.9 ya makadirio. Kati ya mapato yaliyokusanywa **Tsh. 33,731,600** zinatokana na malipo ya leseni za walimu, **Tsh. 241,735,096** za malipo ya usajili wa skuli za binafsi, **Tsh. 8,493,000** kwa ajili ya malipo ya tenda za wazabuni, **Tsh. 311,080,000** usajili wa wanafunzi wa skuli binafsi wanaofanya mitihani ya Taifa pamoja na usajili wa vituo vya kufanyia mitihani na **Tsh. 8,325,400** za makusanyo ya ada za kiingilio kwa wanafunzi wanaojiunga na kidato cha sita.

UTEKELEZAJI WA PROGRAMU KUU NA NDOGO KWA MWAKA 2025/2026.

- 12. Mheshimiwa Spika,** Baada ya kueleza makusanyo ya mapato ya Wizara, sasa naomba kuwasilisha utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo ya Elimu kwa mwaka wa fedha wa 2025/2026 kwa kupitia programu sita za elimu.

MUUNDO WA PROGRAMU

- 13. Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali ina jumla ya programu kuu sita kama zifuatazo: -
Programu ya Kwanza: Elimu ya Maandalizi na Msingi

Programu ya Pili: Elimu ya Sekondari

Programu ya Tatu: Elimu ya Juu

Programu ya Nne: Elimu Mbadala na Mafunzo ya Amali

Programu ya Tano: Ubora wa Elimu

Programu ya Sita: Uongozi na Utawala

- 14. Mheshimiwa Spika,** Utekelezaji wa programu hizi umezingatia malengo ya maendeleo ya elimu katika ngazi ya kitaifa na kimataifa, ikiwemo Dira ya Maendeleo ya Zanzibar ya mwaka 2020–2050, Mpango wa Mageuzi wa Sekta ya Elimu 2023-2030, Ilani ya Chama cha Mapinduzi, pamoja na Maelekezo na ahadi za Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Aidha, programu hizo zimezingatia pia mipango na mikakati mingine ya Kimataifa ikiwemo Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs).
- 15. Mheshimiwa Spika,** programu hizo zote zilitekelezwa kwa mashirikiano makubwa kati ya Serikali, Washirika wa Maendeleo wa ndani na nje ya Zanzibar pamoja na Jamii kwa ujumla. Kwa mwaka wa fedha 2025/2026, Programu hizi zilitengewa jumla ya **TSh. 864,005,977,000**. Kati ya hizo **TSh. 658,281,537,000** ni za SMZ na **TSh. 205,724,440,000** ni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo. Kwa upande wa fedha za SMZ, **TSh. 321,856,000,000** zilitengwa kwa shughuli za miradi ya maendeleo, **TSh. 229,529,200,000** kwa mishahara, **TSh 52,170,037,000** za matumizi mengineyo na **TSh. 54,726,300,000** ni kwa ajili ya ruzuku kwa Taasisi za Wizara zinazopokea ruzuku. Aidha, fedha kutoka kwa

washirika wa maendeleo **TSh. 5,106,800,000** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo na **TSh. 200,617,640,000** ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo

16. **Mheshimiwa Spika**, hadi kufikia Aprili 2026, jumla ya **TSh. 451,717,548,090** sawa na asilimia 52.3 ya makadirio zilipatikana. Jumla ya **TSh. 183,451,360,064** sawa na asilimia 79.9 ya fedha zilizotengwa kwa ajili ya mishahara zimetumika na **TSh 35,953,093,286** zimetumika kwa matumizi mengineyo sawa na asilimia 68.9 ya makadirio ya kutekeleza shughuli hizo. Jumla ya **Tsh 43,308,655,238** zimepatikana kwa Taasisi zinazopokea ruzuku sawa na asilimia 79.1 ya makadirio. Kwa upande wa fedha za maendeleo, jumla ya **TSh. 186,570,054,864** sawa na asilimia 35.7 zilipatikana. Kati ya fedha hizo, TSh. 129,648,912,924 sawa na asilimia 40.3 ya fedha zilizopangwa kwa upande wa Serikali zilipatikana na **TSh. 56,921,141,940** sawa na asilimia 28.4 ya fedha zilizotengwa kwa Washirika wa Maendeleo zimepatikana. Utekelezaji halisi kwa kila Programu ni kama ifuatavyo: -

PROGRAMU YA KWANZA: ELIMU YA MAANDALIZI NA MSINGI

17. **Mheshimiwa Spika**, programu hii inahusisha uimarishaji na utoaji wa elimu ya maandalizi na msingi kwa wanafunzi wenye umri wa kuanzia miaka minne hadi kumi na mbili.
18. **Mheshimiwa Spika**, programu hii ilitengewa jumla ya **TSh. 250,051,036,000**, Kati ya fedha hizo, **TSh. 112,012964,000**

kwa ajili ya mishahara ya wafanyakazi, **TSh. 10,071,622,000** kwa ajili ya matumizi mengineyo na **TSh. 127,966,450,000** kwa miradi ya maendeleo. Hadi kufikia Aprili 2026, jumla ya **TSh. 132,733,212,699** sawa na asilimia 53.1 ya makadirio zilipatikana. Jumla ya **TSh. 86,528,319,326** sawa na asilimia 77.2 ya fedha zilizotengwa kwa ajili ya mishahara zimetumika na **TSh 7,266,820,537** zimetumika kwa matumizi mengineyo sawa na asilimia 72.2 ya makadirio ya kutekeleza shughuli hizo. Kwa upande wa fedha za maendeleo, jumla ya **TSh. 38,938,072,836** sawa na asilimia 31.7 zilipatikana. Kati ya fedha hizo, **TSh. 34,510,049,714** sawa na asilimia 33.0 ya fedha zilizopangwa kwa upande wa Serikali zilipatikana na **TSh. 4,428,023,122** sawa na asilimia 19.0 ya fedha zilizotengwa kwa Washirika wa Maendeleo zimepatikana. Fedha hizo zilitumika kutekeleza shughuli zifuatazo: -

- i) Wizara imeendelea kuimarisha miundombinu ya elimu kwa kuanza ujenzi wa skuli nane za msingi za ghorofa Unguja na Pemba zenye jumla ya madarasa 256. Maeneo yanayojengwa Skuli hizo ni Fuoni Kibondeni, Chunga, Mitiulaya, Minungwini, Mchangamdogo, Wesha, Mtoni Kidatu na Mtopepo. Sambamba na hatua hiyo, Wizara imekamilisha ujenzi wa skuli 21 na kuzifungua rasmi katika maeneo mbalimbali ya Unguja na Pemba zikiwemo skuli 13 za Maandalizi na skuli 8 za Msingi.
- ii) Wizara imeendesha mikutano ya uhamasishaji wa uandikishaji wa watoto wa Maandalizi na Darasa

la Kwanza kwa kushirikiana na viongozi na wadau mbalimbali ambapo jumla ya washiriki 13,322 walifikiwa. Uhamasishaji huo pia ulifanyika kupitia vyombo vya habari pamoja na njia ya simu. Kufuatia uhamasishaji huo, jumla ya wanafunzi wapya 55,895 wameandikishwa ngazi ya maandalizi mwaka wa kwanza na wanafunzi wapya 60,253 kwa ngazi ya msingi darasa la kwanza.

- iii) Wizara imefanya upimaji kwa watoto 5,998 wa Maandalizi mwaka wa Pili, Unguja na Pemba ili kutathmini uwezo wao wa kusoma, kuandika na kuhesabu. Matokeo yanaonesha kuwa kati ya watoto 5,998 waliopimwa, watoto 4,633 sawa asilimia 77.2 walifikia viwango vya ustadi vya kujua kusoma, kuandika na kuhesabu.
- iv) Wizara imeendelea kuimarisha uendeshaji wa skuli kwa kutoa ruzuku kwa skuli 425 za Maandalizi na Msingi Unguja na Pemba. Vilevile, imegharimia huduma za chakula na lishe ambapo wanafunzi 63,099 katika skuli 356 za Maandalizi pamoja na wanafunzi 30,175 wa programu ya lishe wamenufaika sambamba na utoaji wa fedha za chakula kwa dakhalia za Jendele na Pujini.
- v) Wizara imeendelea kuimarisha uwezo wa rasilimali watu kwa kuwapatia watendaji 12 wa Idara ya Elimu Maandalizi na Msingi mafunzo ya muda mfupi kuhusu ufuatiliaji na tathmini pamoja na majukumu na maadili ya utumishi wa umma. Vilevile, mafunzo ya uongozi yalitolewa kwa viongozi wa Serikali za

wanafunzi, walimu na maafisa wa Wizara ambapo jumla ya washiriki 209 walinufaika.

- vi) Wizara ilifanya ziara za ufuatiliaji wa utekelezaji wa shughuli za kila siku katika vituo 122 vya TuTu, skuli 247 za Maandalizi na Msingi pamoja na skuli 52 za Msingi zinazonufaika na mradi wa lische kwa lengo la kuhakikisha huduma hizo zinatekelezwa kwa ufanisi.

Utekelezaji wa Shabaha

- i) Kiwango cha uandikishaji wa wanafunzi wa maandalizi kimefikia asilimia 81.6 mwaka 2026 ikilinganishwa na asilimia 82.5 mwaka 2025.
- ii) Kiwango cha uandikishaji wa wanafunzi katika ngazi ya msingi kimeongezeka kutoka asilimia 103.8 mwaka 2025 hadi kufikia asilimia 107.7 mwaka 2026.
- iii) Uwiano wa wanafunzi kwa mwalimu ngazi ya maandalizi umeendelea kumeimarika na kubaki 27 mwaka 2026 kama ilivyokuwa mwaka 2025.
- iv) Uwiano wa wanafunzi kwa mwalimu ngazi ya msingi umeendelea kumeimarika na kubaki 39 mwaka 2026 kama ilivyokuwa mwaka 2025.
- v) Uwiano wa wanafunzi kwa darasa ngazi ya msingi umepungua kutoka 57 mwaka 2025 hadi kufikia 55 mwaka 2026.

PROGRAMU YA PILI: ELIMU YA SEKONDARI

- 19. Mheshimiwa Spika,** Programu hii inalenga kutoa na kuimarisha elimu ya Sekondari. Kwa mwaka wa fedha

2025/2026, Jumla ya **TSh. 306,480,272,000** zilipangwa kutumika, kati ya fedha hizo **TSh. 100,097,637,000** ni kwa ajili ya malipo ya mishahara ya wafanyakazi, **TSh. 23,984,521,000** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo na jumla ya **TSh. 182,398,114,000** kwa kazi za maendeleo. Hadi kufikia Aprili 2026, jumla ya **TSh. 169,267,554,724** sawa na asilimia 55.2 ya makadirio zilipatikana. Jumla ya **TSh. 81,123,164,845** sawa na asilimia 81.0 ya fedha zilizotengwa kwa ajili ya mishahara zimetumika na **TSh 17,296,576,702** zimetumika kwa matumizi mengineyo sawa na asilimia 72.1 ya makadirio ya kutekeleza shughuli hizo. Kwa upande wa fedha za maendeleo, jumla ya **TSh. 70,847,813,177** sawa na asilimia 38.8 zilipatikana. Kati ya fedha hizo, **TSh. 50,441,316,736** sawa na asilimia 50.2 ya fedha zilizopangwa kwa upande wa Serikali zilipatikana na **TSh. 20,406,496,441** sawa na asilimia 24.9 ya fedha zilizotengwa kwa Washirika wa Maendeleo zimepatikana. Fedha hizo zilitumika kutekeleza shughuli zifuatazo: -

- i) Wizara imeratibu na kusimamia uendeshaji wa Mtihani wa Taifa wa Kidato cha Nne kwa mwaka 2025 ambapo wanafunzi 21,098 walifanya mtihani huo. Kati yao, watahiniwa 19,075 sawa na asilimia 90.4 walifaulu. Ufaulu huu ni sawa na ongezeko la asilimia 8.4 ikilinganishwa na matokeo ya mwaka 2024.
- ii) Wizara imeanza ujenzi wa Skuli saba za Sekondari za ghorofa Unguja na Pemba, zenye jumla ya madarasa 179. Maeneo yanayojengwa Skuli hizo ni Jumbi, Kianga, Mikunguni, Jang'ombe kwa Unguja na Micheweni, Vitongoji na Kengeja kwa Pemba. Sambamba na

hatua hiyo, Wizara imekamilisha ujenzi wa skuli 13 na kuzifungua rasmi katika maeneo mbalimbali ya Unguja na Pemba.

- iii) Wizara imeendelea kutoa fedha za uendeshaji kwa dakhalia 22 zenye wanafunzi 11,772, pamoja na ruzuku kwa skuli 231 za sekondari na hubs 22 za ubunifu wa kisayansi Unguja na Pemba. Aidha, imenunua na kusambaza magodoro mapya 3,586 katika dakhalia 17 ili kuboresha mazingira ya malazi kwa wanafunzi.
- iv) Wizara imesambaza vifaa vya kufundishia na kujifunzia vikiwemo vya masomo ya ufundi kwa Skuli za Ufundi za Mikunguni na Kengeja, vifaa vya maabara kwa skuli 205 pamoja na mahitaji muhimu ya ufundishaji kama madaftari ya mahudhurio, chaki na kadi za maendeleo. Aidha, vifaa vya utekelezaji wa Mtaala mpya wa Mafunzo ya Amali vimesambazwa katika skuli 14, vikiwemo vifaa vya umeme, uhunzi, upishi, useremala, kilimo, michezo, sanaa, kompyuta, ushoni na masomo mengine ya vitendo.
- v) Wizara imeendelea kuimarisha mazingira ya kufundishia na kujifunzia kwa kuanza kuweka miundombinu ya gesi ya kupikia katika dakhalia 17 za Unguja na Pemba. Aidha, katika kuimarisha usalama wa mazingira ya skuli, kemikali chakavu zimeondoshwa katika skuli 30 za sekondari.
- vi) Wizara imeendelea kuimarisha uwezo wa walimu katika utekelezaji wa mtaala kwa kuwajengea uwezo walimu 349 kuhusu Mtaala mpya wa umahiri. Walimu hao wanajumuisha walimu wapya 70, walimu wakuu 93,

wasaidizi walimu wakuu 93 na wakuu wa seksheni 93. Vilevile, jumla ya walimu 1,014 na wanafunzi 20,137 kutoka skuli 78 za sekondari za Unguja na Pemba wamenufaika na mafunzo ya uhamasishaji wa masomo ya sayansi na ubunifu. Aidha, wanafunzi 675 walishiriki mashindano ya sayansi katika ngazi za Wilaya na Mikoa.

Utekelezaji wa Shabaha

- i) Kiwango cha uandikishaji wa wanafunzi wa sekondari (kidato cha 1 - 4) kimeimarika kutoka asilimia 68.2 mwaka 2025 hadi kufikia 80.2 mwaka 2026.
- ii) Kiwango cha ufaulu wa wanafunzi wa kidato cha nne kimeongezeka kutoka asilimia 82 mwaka 2024 hadi kufikia asilimia 90.4 mwaka 2025.
- iii) Kiwango cha ufaulu wa wanafunzi wa kidato cha sita kimefikia asilimia 99.8 mwaka 2025 ikilinganishwa na asilimia 99.9 mwaka 2024.
- iv) Wastani wa uwiano wa wanafunzi kwa darasa ngazi ya Sekondari umeongezeka kutoka 45 mwaka 2025 na kufikia 50 mwaka 2026.

PROGRAMU YA TATU: ELIMU YA JUU

20. Mheshimiwa Spika, Madhumuni ya programu ya Elimu ya Juu ni kutoa elimu itakayomuwezesha muhitimu kujijajiri au kuajiriwa. Programu hii ina programu ndogo moja ya mafunzo ya ualimu na maeneo matano ya huduma, ikiwemo Huduma ya Ushauri na Utafiti; Huduma ya Sayansi na Teknolojia, Huduma ya Teknolojia – IIT Madras, Huduma ya Mikopo ya Elimu ya Juu na Huduma ya Uratibu wa Elimu

ya Juu. Programu hii ilipangiwa **TSh. 157,267,238,000**, kati ya fedha hizo **TSh. 31,310,109,450** ni kwa ajili ya malipo ya mishahara ya wafanyakazi, **Tsh. 6,813,459,550** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo na **TSh. 119,143,669,000** zilitengwa kwa shughuli za maendeleo. Hadi kufikia April, 2026 jumla ya **TSh. 82,353,036,725** sawa na asilimia 52.4 ya makadirio zilipatikana. Jumla ya **TSh. 25,839,896,379** sawa na asilimia 82.5 ya fedha zilizotengwa kwa ajili ya mishahara zimetumika na **TSh 3,369,149,746** zimetumika kwa matumizi mengineyo sawa na asilimia 49.4 ya makadirio ya kutekeleza shughuli hizo. Kwa upande wa fedha za maendeleo, jumla ya **TSh. 53,143,990,600** sawa na asilimia 44.6 zilipatikana. Kati ya fedha hizo, **TSh. 36,701,762,667** sawa na asilimia 48.9 ya fedha zilizotengwa kwa shughuli za maendeleo zimepatikana kutoka Serikalini na **TSh. 16,442,227,933** sawa na asilimia 37.3 ya fedha zilizopangwa kutumika kwa upande wa Washirika wa Maendeleo zimepatikana. Utekelezaji halisi wa programu hii ni kama ifuatavyo:

Programu ndogo ya Mafunzo ya Ualimu

- 21. Mheshimiwa Spika**, Madhumuni makubwa ya Programu hii ni kuwawezesha walimu kuwa wabunifu, wataalamu na wenye uwezo wa kuongoza ili kukuza ubora wa elimu. Programu hii ndogo inatekelezwa na Idara ya Mafunzo ya Ualimu. Kwa mwaka wa fedha 2025/2026 programu hii ilipangiwa kutumia jumla ya **Tsh. 6,638,469,000**. Kati ya fedha hizo, **TSh. 3,230,309,450** ni kwa ajili ya malipo

ya mishahara ya wafanyakazi, **TSh. 908,159,550** ni kwa matumizi ya mengineyo na **TSh. 2,500,000,000** ni kwa ajili ya kazi za Maendeleo. Hadi kufikia Aprili 2026, jumla ya **TSh. 3,678,391,646** sawa na asilimia 55.4 ya makadirio zilipatikana. Jumla ya **TSh. 2,866,867,593** sawa na asilimia 88.7 ya fedha zilizotengwa kwa ajili ya mishahara zimetumika na **TSh 811,524,053** zimetumika kwa matumizi mengineyo sawa na asilimia 89.4 ya makadirio ya kutekeleza shughuli hizo. Fedha hizo zilitumika kutekeleza shughuli zifuatazo: -

- i) Wizara imetoa mafunzo endelevu kazini (CPD) na namafunzo endelevu kazini katika ngazi ya skuli (SBI) kwa washauri wa masomo 33, walimu wakuu na wasaidizi wao 314, pamoja na wakuu wa masomo 495 kuhusu usimamizi wa mafunzo hayo skuli. Aidha, walimu 1,231 wamepatiwa mafunzo ya SBI yaliyolenga utekelezaji wa mtaala wa umahiri, mbinu za ufundishaji, matumizi ya kompyuta, maandalizi ya vifaa vya kufundishia, utayarishaji wa madaftari ya kazi na matumizi ya nidhamu endelevu darasani.
- ii) Wizara imeendelea kuimarisha mfumo wa ufuatiliaji na usimamizi wa ufundishaji kwa kuwapatia mafunzo ya mbinu za ufuatiliaji na tathmini waratibu na washauri wa masomo 113 wa skuli za Maandalizi, Msingi na Sekondari Unguja. Aidha, ziara 2,138 za ufuatiliaji zimefanyika Unguja na Pemba ambapo walimu 7,481 wamefuatiliwa na kupatiwa ushauri wa kitaaluma unaostahiki.

- iii) Wizara imetoa mafunzo ya kuwajengea uwezo walimu wapya 420 kuhusu mtaala unaozingatia umahiri na namna ya kuandaa vifaa vya mtaala, ili waweze kutekeleza majukumu ya ujifunzaji na ufundishaji kwa ufanisi zaidi.
- iv) Wizara imeanza utayarishaji wa muongozo wa uendeshaji wa Vituo vya Walimu kwa kufanya vikao saba vya kukusanya maoni ya wadau Unguja na Pemba, vilivyohusisha washiriki 244 kutoka taasisi mbalimbali za sekta ya elimu.
- v) Wizara imeendesha mafunzo ya siku 15 ya moduli za masomo ya Sayansi kwa walimu 1,749 wa masomo ya Sayansi na Kiingereza wa Skuli za Msingi na Sekondari Unguja na Pemba.
- vi) Wizara inaendelea na ukarabati wa vyuo vya ualimu vya Mazizini na Kiuuyu, ambapo kazi imefikia asilimia 72 katika Chuo cha Mazizini na asilimia 55 katika Chuo cha Kiuuyu.

Utekelezaji wa Shabaha

- i) Jumla ya Wanafunzi 163 wamejiunga na vyuo vya mafunzo ya Ualimu vya CCK Mazizini, Kiuuyu Pemba na Nkrumah.
- ii) Asilimia ya walimu wenye sifa imeongezeka kutoka asilimia 96 mwaka 2024 hadi kufikia asilimia 100 mwaka 2025.
- iii) Idadi ya Wanafunzi waliohitimu mafunzo ya Ualimu katika ngazi ya Astashahada na Stashahada imeongezeka kutoka 1,290 mwaka 2024 hadi kufikia 1,837 mwaka 2025.

- iv) Idadi ya Walimu waliopatiwa mafunzo kazini imeongezeka kutoka 3,028 mwaka 2024 hadi kufikia 5,460 mwaka 2025.
- v) Idadi ya Walimu waajiriwa wavya waliopatiwa mafunzo imeongezeka kutoka 252 mwaka 2024 hadi kufikia 420 kwa mwaka 2025.

Huduma ya Elimu ya Juu, Ushauri na Utafiti

- 22. Mheshimiwa Spika**, huduma ya Elimu ya Juu, Ushauri na Utafiti ina lengo la kuwaandaa wanafunzi kuingia katika fani za kitaalamu na ajira. Huduma hii inatolewa kupitia Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA).
- 23. Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka wa fedha 2025/2026, SUZA ilitengewa ruzuku ya **TSh. 68,542,346,000**, Kati ya fedha hizo **TSh. 19,543,700,00** kwa ajili ya ruzuku ya mishahara na **TSh. 48,998,646,000** kwa shughuli za maendeleo kati ya fedha hizo **TSh 14,000,000,000** ni kutoka SMZ na **TSh 34,998,646,000** ni kutoka kwa Washirika Wamaendeleo. Hadi kufikia Aprili 2026, jumla ya **TSh. 33,932,607,101** sawa na asilimia 49.5 zimepatikana. Kati ya fedha hizo, jumla ya **TSh. 15,706,800,527** sawa na asilimia 80.4 ya fedha zilizotengwa kwa ajili ya mishahara zimetumika. Kwa upande wa fedha za maendeleo, jumla ya **TSh. 18,225,806,574** zilipatikana sawa na asilimia 37.2. Kati ya fedha hizo, **TSh. 2,251,054,000** sawa na asilimia 16.1 ya fedha zilizopangwa kwa upande wa Serikali zilipatikana na **TSh. 15,974,752,574** sawa na asilimia 45.6 ya fedha zilizotengwa kwa Washirika wa Maendeleo zimepatikana. Utekelezaji halisi wa huduma hii ni kama ifuatavyo: -

- i) Jumla ya wanafunzi wapya 2,976 wamedahiliwa kujiunga na masomo katika ngazi mbalimbali, kati ya hao wanafunzi 430 wamejiunga na Astashahada, 813 Stashahada, 1,638 Shahada ya kwanza, 96 Shahada ya uzamili na wawili Shahada ya Uzamivu.
- ii) Jumla ya wanafunzi 2,536 wamehitimu na kutunukiwa vyeti katika ngazi mbalimbali kuanzia Astashahada hadi Shahada ya Uzamivu. Wahitimu hao wanajumuisha Shahada ya Uzamivu saba, Shahada ya Uzamili 90, Shahada ya Kwanza 986, Stashahada 1,143 na Astashahada 317.
- iii) Wizara imeendelea kuimarisha miundombinu ya SUZA na taasisi zake kupitia ujenzi wa maabara ya sayansi na jengo la Skuli ya Kilimo chini ya Mradi wa HEET, pamoja na kuanza maandalizi ya ujenzi wa jengo la utawala, kituo cha wanafunzi, Skuli ya Elimu, nyumba za wafanyakazi na kiwanja cha michezo kupitia mradi wa BADEA. Aidha, ujenzi wa dakhalia za wanafunzi, Taasisi ya Ubaharia na uzio wa Kampasi ya Benjamin Mkapa Pemba unaendelea.
- iv) Wizara imeendelea kuwajengea uwezo watumishi wake kwa kuwapatia mafunzo ya muda mrefu ndani na nje ya nchi wafanyakazi 116 katika ngazi za Shahada ya Kwanza (17), Uzamili (38) na Uzamivu (61), pamoja na kutoa mafunzo ya muda mfupi kwa wafanyakazi 24 katika maeneo mbalimbali ya kiutendaji. Aidha, katika kuimarisha shughuli za utafiti, wanataaluma 45 wamepatiwa mafunzo ya utafiti.

- v) Wizara imesimamia zoezi la mafunzo ya kazi za vitendo katika Wizara na Taasisi mbali mbali ambapo jumla ya wanafunzi 2,654 walishiriki pamoja na kusimamia kazi za wanafunzi (projects) wanaomaliza ngazi za Stashahada, Shahada za kwanza na ya pili katika fani tofauti.
- vi) Wizara imeendelea kuimarisha mitaala na programu za masomo kwa kupitisha mitaala saba na kuziwasilisha TCU kwa ajili ya ithibati sambamba na kuandaa mitaala mipya ya Shahada ya Ufamasia, Aquaculture na Fisheries pamoja na kuanza maandalizi ya mtaala wa Data Science and Applied Artificial Intelligence. Aidha, mtaala wa mafunzo ya lazima ya baharini (STCW) umewasilishwa Seneti kwa hatua zaidi. Katika hatua nyengine, Wizara imeanzisha Shahada ya Uzamili ya Kiarabu iliyodahili wanafunzi 14 katika mwaka wa masomo 2025/2026.

Utekelezaji wa Shabaha

- i) Idadi ya Wanafunzi wanaomaliza ngazi mbalimbali za uzamivu, uzamili, shahada, stashahada na astashahada imeongezeka kutoka 2,291 mwaka 2025 hadi kufikia 2,536 mwaka 2026.
- ii) Programu mpya za masomo zimeongezeka kutoka programu nne mwaka 2024/2025 hadi kufikia programu 12 mwaka 2025/2026
- iii) Idadi ya tafiti zilizofanywa imeongezeka kutoka tafiti 12 zilizofanywa mwaka 2024/2025 hadi kufikia 18 kwa mwaka 2025/2026.

- iv) Idadi ya wanafunzi wapya waliodahiliwa imeongezeka kutoka wanafunzi 2,326 mwaka 2024/2025 hadi kufikia wanafunzi 2,976 mwaka 2025/2026.

Huduma ya Sayansi na Teknolojia

24. Mheshimiwa Spika, huduma ya Sayansi na Teknolojia ni miongoni mwa huduma muhimu katika kuinua kiwango cha Elimu ya Uhandisi, Sayansi na Teknolojia na kuimarisha maendeleo ya uchumi wa nchi. Shughuli za huduma hii zinatekelezwa na Taasisi ya Karume ya Sayansi na Teknolojia. Kwa mwaka 2025/2026, Taasisi hii ilitengewa ruzuku ya **TSh. 18,568,823,000**, Kati ya fedha hizo **TSh. 3,484,800,000** zilitengwa kwa ajili ya ruzuku ya mishahara na **TSh. 15,084,023,000** kwa kazi za maendeleo, kati ya fedha hizo **TSh 6,000,000,000** ni kutoka SMZ na **TSh 9,084,023,000** ni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo. Hadi kufikia April 2026, jumla ya **TSh. 10,645,782,755** sawa na asilimia 57.3 ya makadirio zilipatikana. Jumla ya **TSh. 3,042,449,207** sawa na asilimia 87.3 ya fedha zilizotengwa kwa ajili ya mishahara zimetumika. Kwa upande wa fedha za maendeleo, jumla ya **TSh. 7,603,333,549** sawa na asilimia 41.9 zilipatikana. Kati ya fedha hizo, **TSh. 7,135,858,190** sawa na asilimia 118.9 ya fedha zilizopangwa kwa upande wa Serikali zilipatikana na **TSh. 467,475,359** sawa na asilimia 5.1 ya fedha zilizotengwa kwa Washirika wa Maendeleo zimepatikana. Utekelezaji halisi wa shughuli za huduma hii ni kama ifuatavyo:

- i) Wizara imetoa mafunzo ya ujasiriamali kwa wajasiriamali 40, waendesha boda boda na bajaji 56, na washiriki 100

wa mafunzo ya kompyuta. Kwa upande wa watumishi, jumla ya watumishi 35 wanaendelea na mafunzo ya muda mrefu katika ngazi mbalimbali za elimu ndani na nje ya nchi kupitia ufadhili wa mradi wa SEBEP. Aidha, wakufunzi 12 na wanafunzi 13 wa KIST wamepatiwa mafunzo ya Data Science and Artificial Intelligence ili kuimarisha ujuzi wa kidijitali na kitaaluma.

- ii) Wizara imeshiriki katika Maonesho ya Wiki ya Elimu ya Juu na Maonesho ya Nane Nane, na hivyo kufanikisha kuitangaza Taasisi pamoja na shughuli zake kwa zaidi ya watu 5,000 waliotembelea banda lake. Uhamasishaji huo umezaa matunda kwa kuwezesha udahili wa wanafunzi 185 kujiunga na Taasisi.
- iii) Wizara imefanikiwa kupokea vifaa vya kufundishia na kujifunzia vya Internet of Things (IoT) na Artificial Intelligence (AI) kutoka Mradi wa AHUMAIN vyenye thamani ya Euro 16,605.
- iv) Wizara imefungua rasmi Tawi la KIST, Pemba ambapo kupitia tawi hilo vijana 224 wamepatiwa mafunzo ya muda mfupi ya boda boda, bajaji na kompyuta kwa lengo la kuwawezesha kujiajiri au kuajiriwa. Aidha, mafunzo ya muda mrefu katika fani za umeme na kompyuta yameanza kutolewa, ambapo wanafunzi 38 wanaendelea na masomo.

Utekelezaji wa Shabaha

- i) Jumla ya wanafunzi 1,401 wa fani za Ufundi, Uhandisi, Sayansi, Teknolojia na Mafunzo ya Amali wameandikishwa kwa mwaka 2025/2026.
- ii) Idadi ya wahitimu wa fani za Ufundi, Uhandisi, Sayansi,

Teknolojia na Mafunzo ya Amali imeongezeka kutoka 940 mwaka 2024/2025 na kufikia 1,039 mwaka 2025/2026.

Huduma ya Teknolojia – IIT Madras

25. Mheshimiwa Spika, Huduma ya Teknolojia – IIT Madras ina lengo la kuwaandaa wanafunzi katika elimu ya Sayansi na Teknolojia kuingia katika fani za kitaalamu na ajira. Huduma hii inatolewa katika Taasisi ya Teknolojia ya India. Kwa mwaka wa fedha 2025/2026, Jumla ya **TSh. 21,061,000,000** zilipangwa kutumika, kati ya fedha hizo **TSh. 3,500,000,000** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo na **TSh. 17,561,000,000** kwa kazi za maendeleo. Hadi kufikia Aprili 2026, jumla ya **TSh. 5,455,569,999** sawa na asilimia 30.0 zimepatikana. Jumla ya **TSh. 1,640,719,522** sawa na asilimia 46.9 ya fedha zilizotengwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida zimetumika. Kwa upande wa fedha za Maendeleo, jumla ya **TSh. 3,814,850,477** sawa na asilimia 21.7 ya fedha zilizotengwa kwa shughuli za maendeleo zilipatikana kutoka Serikalini. Utekelezaji halisi wa shughuli za huduma hii ni kama ifuatavyo:

- i) Jumla ya wanafunzi wapya 47 (Wanaume 30 na wanawake 17) wamedahiliwa kujiunga na masomo katika ngazi ya Shahada ya kwanza na Shahada ya uzamili.
- ii) Ujenzi wa utanuzi wa Chuo cha IITM unaendelea katika hatua ya ujenzi wa dakhalia kwa sasa umefikia asilimia 92.

Huduma ya Mikopo ya Elimu ya Juu

- 26. Mheshimiwa Spika,** Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu Zanzibar inatekeleza majukumu makuu matatu, ambayo ni kutoa mikopo kwa wanafunzi wahitaji wenye sifa za kujiunga na masomo ya elimu ya juu; kusimamia na kufuatilia nafasi za ufadhili wa masomo kutoka kwa washirika mbalimbali wa maendeleo ndani na nje ya Tanzania na kukusanya marejesho ya mikopo ya wanafunzi kutoka kwa wanufaika wote.
- 27. Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa fedha 2025/2026, jumla ya **TSh. 37,945,700,000** zilitengwa. Kati ya fedha hizo **TSh. 2,945,700,000** kwa ajili ya ruzuku ikiwemo **TSh. 834,100,000** ruzuku ya mishahara, **TSh. 2,111,600,000** kwa matumizi mengineyo na **TSh. 35,000,000,000** zilitengwa kwa ajili ya kutoa mikopo kwa wanafunzi wapya na wanaoendelea na masomo ya Elimu ya Juu. Hadi kufikia Aprili 2026, jumla ya **TSh. 25,007,666,173** sawa na asilimia 65.9 ya makadirio zilipatikana. Jumla ya **TSh. 742,362,840** sawa na asilimia 89.0 ya fedha zilizotengwa kwa ajili ya mishahara zimetumika na **TSh 765,303,333** zimepatikana sawa na asilimia 36.2 ya fedha za matumizi mengineyo. Kwa upande wa fedha za maendeleo, jumla ya **TSh. 23,500,000,000** zilipatikana kutoka Serikalini sawa na asilimia 67.1 ya fedha zilizotengwa kwa shuguli za maendeleo. Utekelezaji halisi wa huduma hii ni kama ifuatavyo: -

- i) Jumla ya wanafunzi 18,593 wamepatiwa mikopo ya elimu ya juu wakiwemo wanafunzi wapya 8,975 na 9,618 wanaoendelea na masomo katika vyuo vya ndani na nje ya Tanzania. Ongezeko la wanafunzi 4,098 wapya walioteuliwa inatokana na kuongezeka kwa ufaulu wa wanafunzi wa kidato cha sita, kuwepo kwa dirisha jipya la ngazi ya stashahada, na ongezeko la maombi wa mkopo kwa wanafunzi wapya.
- ii) Wizara imefanya uhamasishaji kwa jamii kuhusu uombaji na urejeshaji wa mikopo kupitia maonesho ya wiki ya Juma la Elimu ya Juu (Unguja na Pemba), maonesho ya Nane nane Dole. Aidha, vyombo vya habari vilitumika vikiwemo gazeti la Zanzibar leo, ZBC Radio, ZBCTV, ZANZIBAR CABLE na mitandao ya kijamii.
- iii) Wizara imeendelea kutoa ufadhili wa masomo kupitia Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa wanafunzi bora wa Kidato cha Sita, ambapo jumla ya wanafunzi 335, wakiwemo 117 wapya na 218 wanaoendelea na masomo, wamenufaika. Aidha, wanafunzi wapya 59 wamepatiwa ufadhili wa masomo katika vyuo vya ndani ya nchi kupitia taasisi za Darul Iman na Direct Aid.
- iv) Wizara imefanikiwa kufanya uhakiki wa wanafunzi 9,258 katika vyuo vya ndani ya Tanzania na kuwaunganisha wanafunzi 8,975 na huduma ya bima ya afya.

Utekelezaji wa Shabaha

- i) Idadi ya Wanafunzi wapya waliopatiwa mkopo wa Elimu ya Juu imeongezeka kutoka wanafunzi 7,198 kwa mwaka 2024/2025 hadi kufikia wanafunzi 8,975 kwa mwaka 2025/2026.
- ii) Makusanyo ya marejesho ya mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu yamefikia TSh 4.6 bilioni mwaka 2026 ikilinganishwa na TSh 5.5 bilioni mwaka 2026.
- iii) Idadi ya wanafunzi waliopatiwa ufadhili wa SMZ imeongezeka kutoka wanafunzi 75 mwaka 2024/2025 hadi kufikia wanafunzi 117 kwa mwaka 2025/2026.

Huduma ya Uratibu wa Elimu ya Juu

28. Mheshimiwa Spika, huduma hii ina jukumu la kusimamia na kutathmini maendeleo ya elimu ya juu na inatekelezwa na Kitengo cha Uratibu wa Elimu ya Juu. Kwa mwaka wa fedha 2025/2026, Kitengo kilitengewa jumla ya TSh. 150,000,000 kutoka Serikalini kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Hadi kufikia Aprili 2026, jumla ya **Tsh. 60,902,000** sawa na asilimia 40.6 zimepatikana. Utekelezaji halisi ni kama ifuatavyo: -

- i) Wizara imefanya ufuatiliaji na tathmini katika taasisi 12 za elimu ya juu na kati kwa lengo la kufuatilia utoaji wa huduma, uendeshaji wake na uzingatiaji wa sheria na kanuni zilizowekwa. Matokeo ya ufuatiliaji huo yanaonesha kuwa taasisi zote zilizotembelewa zimesajiliwa kisheria na zinaendesha shughuli zake kwa kuzingatia taratibu.

- ii) Wizara imeendelea kuratibu na kutangaza fursa za masomo ya udhamini kutoka takribani nchi 19 pamoja na taasisi na programu mbalimbali za kimataifa kwa ngazi ya Shahada, Shahada ya Uzamili na Uzamivu. Aidha, Wizara ilishiriki katika uchambuzi na tathmini ya maombi ya nafasi hizo, ikiwemo mpango wa Samia Scholarship Extended, Commonwealth Scholarship, pamoja na nafasi za masomo kutoka China na Hungary, kwa lengo la kuhakikisha wanafunzi wenye sifa wanapata fursa hizo.
- iii) Wizara imetoa mafunzo kwa kamati za skuli na wanafunzi kuhusu uchaguzi wa masomo unaoendana na mahitaji ya soko la ajira pamoja na elimu ya jinsia. Mafunzo hayo yaliwahusisha wanafunzi 5,463 na wajumbe 63 wa kamati za skuli.
- iv) Wizara ilifanya maonesho ya sita ya Wiki ya Elimu ya Juu, ambapo taasisi 80 zilishiriki Unguja na 54 Pemba kwa lengo la kutangaza huduma na programu zao kwa wadau. Maonesho hayo yalitembelewa na wadau 24,549 Unguja na 12,561 Pemba

Utekelezaji wa Shabaha

- i. Jumla ya wanafunzi 26,481 wanaendelea na masomo katika vyuo vikuu na vyuo vya kati vilivyopo Zanzibar, kati yao wanaume ni 9,903 na wanawake ni 16,578.

PROGRAMU YA NNE: ELIMU MBADALA NA MAFUNZO YA AMALI

29. Mheshimiwa Spika, programu hii ina madhumuni ya kuwajengea uwezo vijana katika ushindani wa soko la ajira kwa kuwapatia mafunzo mbadala na amali. Programu hii ina programu ndogo mbili; Mafunzo ya Amali na Elimu Mbadala na Watu Wazima. Programu ilitengewa Jumla ya **TSh. 36,651,488,000**, kati ya fedha hizo **TSh. 6,005,528,250** ni kwa ajili ya malipo ya mishahara ya wafanyakazi, **Tsh. 5,785,959,750** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo na jumla ya **TSh. 24,860,000,000** zilitengwa kwa shughuli za maendeleo. Hadi kufikia Aprili 2026, jumla ya **TSh. 11,466,760,909** sawa na asilimia 31.1 ya makadirio zilipatikana. Jumla ya **TSh. 5,048,847,111** sawa na asilimia 84.1 ya fedha zilizotengwa kwa ajili ya mishahara zimetumika na **TSh. 4,199,898,174** zimetumika kwa matumizi mengineyo sawa na asilimia 72.6 ya makadirio ya kutekeleza shughuli hizo. Kwa upande wa fedha za maendeleo, jumla ya **TSh. 2,218,015,624** zilipatikana sawa na asilimia 8.9. Kati ya fedha hizo, **TSh. 1,010,971,000** sawa na asilimia 17.3 ya fedha zilizotengwa kwa shughuli za maendeleo kwa upande wa Serikali zimetumika na **TSh. 1,207,044,624** sawa na asilimia 6.4 ni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo zimepatikana. Utekelezaji halisi wa programu hii ni kama ifuatavyo: -

Programu ndogo ya Elimu Mbadala na Watu Wazima

30. Mheshimiwa Spika, programu hii inatekelezwa na Idara ya Elimu Mbadala na Watu Wazima na ina lengo la kupunguza kiwango cha wasiojua kusoma, kuandika na kuhesabu kwa wanajamii. Kwa mwaka wa fedha 2025/2026, programu hii ilitengewa jumla ya **TSh. 4,640,288,000**, kati ya fedha hizo **TSh. 1,899,528,250** kwa ajili ya mishahara, **TSh. 940,759,750** kwa ajili ya matumizi mengineyo na **TSh. 400,000,000** ni kwa ajili ya maendeleo na **Tsh. 1,400,000,000** ni matumizi mengineyo kutoka kwa wahisani. Hadi kufikia Aprili 2026, jumla ya **TSh. 2,968,087,133** sawa na asilimia 64.0 ya makadirio zilipatikana. Jumla ya **TSh. 1,766,219,949** sawa na asilimia 93.0 ya fedha zilizotengwa kwa ajili ya mishahara zimetumika na **Tsh 1,190,896,184** zimetumika kwa matumizi mengineyo sawa na asilimia 50.9 ya makadirio ya kutekeleza shughuli hizo. Kwa upande wa maendeleo jumla ya **Tsh 10,971,000** zimetumika sawa na asilimia 2.7 ya makadirio. Utekelezaji halisi wa shughuli za programu hii ni kama ifuatavyo: -

- i) Wizara imefanya upimaji mkuu wa mwaka kwa wanafunzi 6,073, ambapo wanafunzi 5,149 sawa na asilimia 85 walifaulu. Aidha, jumla ya wanafunzi 542, wakiwemo wanaume 493 na wanawake 49, walikombolewa sawa na asilimia 82.
- ii) Wizara imefanikiwa kununua vifaa vya kufundishia na kujifunzia kwa walimu na wanakisomo wa Wilaya zote za Unguja. Vifaa vyenyewe ni mbao, Madaftari, chaki na notebook.

- iii) Wizara imeendelea na utaratibu wa kuwalipa posho za mwezi walimu wanaofundisha madarasa ya kisomo Unguja na Pemba. Jumla ya walimu 535 wamenufaika na posho hizo.
- iv) Wizara imefanya mafunzo ya kuwajengea uwezo walimu 300 wanaofundisha madarasa ya kisomo cha watu wazima kwa lengo la kuwaongezea ujuzi na mbinu za ufundishaji zinazolenga kuimarisha ubora wa elimu kwa watu wazima.
- v) Wizara imefanya maadhimisho ya Wiki ya Elimu ya Watu Wazima ambapo kwa mwaka huu maadhimisho hayo yamefanyika Pemba. Jumla ya washiriki 700 walihudhuria maadhimisho hayo

Utekelezaji wa Shabaha

- i) Jumla ya wanafunzi 859 wenye umri kati ya miaka 7 hadi 14 wamerejeshwa skuli mwaka 2025/2026.
- ii) Jumla ya watu wazima 756 wamejiunga katika madarasa ya wanakisomo mwaka 2025.
- iii) Jumla ya vijana 213 wenye umri kati ya miaka 15 hadi 22 waliokosa fursa ya masomo wameandikishwa katika Vituo vya Elimu Mbadala.

Programu ndogo ya Mafunzo ya Amali

- 31. Mheshimiwa Spika**, Programu ndogo ya Mafunzo ya Amali inatekelezwa na Mamlaka ya Mafunzo ya Amali (MMA). Programu hii ndogo ilitengewa jumla ya ruzuku ya **TSh. 32,011,200,000**, Kati ya fedha hizo, **TSh. 7,551,200,000** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo ikiwemo **TSh.**

4,106,000,000 kwa ajili ya mshahara, **Tsh. 3,445,200,000** kwa ajili ya matumizi mengineyo na **TSh. 24,460,000,000** ni kwa ajili ya maendeleo. Hadi kufikia Aprili 2026, jumla ya **TSh. 8,498,673,777** sawa na asilimia 26.5 ya makadirio zilipatikana. Jumla ya **TSh. 3,282,627,163** sawa na asilimia 79.9 ya fedha zilizotengwa kwa ajili ya mishahara zimetumika na **TSh 3,009,001,990** zimetumika kwa matumizi mengineyo sawa na asilimia 87.3 ya makadirio ya kutekeleza shughuli hizo. Kwa upande wa fedha za maendeleo, jumla ya **TSh. 2,207,044,624** zilipatikana sawa na asilimia 9.0. Kati ya fedha hizo, **TSh. 1,000,000,000** sawa na asilimia 18.3 ya fedha zilizopangwa kwa upande wa Serikali zilipatikana na **TSh. 1,207,044,624** sawa na asilimia 6.4 ya fedha zilizotengwa kwa Washirika wa Maendeleo zimepatikana. Utekelezaji halisi ni kama ifuatavyo: -

- i) Wizara imeendelea kuimarisha miundombinu ya MMA kwa kuendelea na ujenzi na ukarabati wa majengo yake, ikiwemo kituo cha afya katika Chuo cha Mafunzo ya Amali Mkokotoni ambacho ujenzi wake umefikia asilimia 70. Aidha, maandalizi ya ujenzi wa Ofisi mpya ya Makao Makuu ya MMA Kisakasaka yanaendelea, ambapo michoro ya kimuundo na BOQ tayari imekamili na hatua za kumpata mkandarasi zinaendelea.
- ii) Wizara imefanya warsha ya maandalizi, uandishi, uhakiki na upangaji wa mitihani ya Taifa kwa lengo la kuimarisha ubora wa mafunzo yatolewayo na MMA. Warsha hii iliwahusisha wakufunzi 36 kutoka vyuo mbalimbali vya Mafunzo ya Amali. Aidha, vifaa na malighafi za mitihani ya vitendo (practical exams)

zilinunuliwa na kusambazwa katika vyuo vitano vya MMA vilivyopo Unguja na Pemba.

- iii) Wizara imekagua na kusajili vituo 14 vipya vya Mafunzo ya Amali, na kufanya ukaguzi katika vyuo na vituo 39 vya mafunzo ya amali Unguja na Pemba ili kuhakikisha vinafuata vigezo vya utoaji wa mafunzo hayo. Ukaguzi huo umewezesha kubaini maeneo yanayohitaji kuimarishwa, hususan upatikanaji wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia.
- iv) Wizara imeendelea kutoa mikopo midogo midogo kwa wahitimu 32 waliounda vikundi kwa lengo la kuwawezesha kujijiri. Aidha, vikundi 12 vilivyopokea mikopo vilifuatiliwa ili kutathmini maendeleo ya shughuli zao, kubaini changamoto zinazowakabili na kuhimiza urejeshaji wa mikopo kwa wakati.
- v) Wizara imewajengea uwezo wafanyakazi, wakufunzi na vijana kupitia mafunzo mbalimbali, ambapo wafanyakazi 37 wanaendelea na masomo ya muda mrefu ndani na nje ya nchi, na wafanyakazi 106 wamepatiwa mafunzo ya muda mfupi kupitia mradi wa SEBEP. Aidha, wakufunzi zaidi ya 86, pamoja na wakufunzi 14 kutoka vyuo vitano vya Mafunzo ya Amali, wamenufaika na mafunzo ya kitaaluma, kiufundi na kimbinu kupitia Kituo cha Umahiri cha Mkokotoni chini ya mradi wa ILO. Vilevile, kwa kushirikiana na taasisi mbalimbali, vijana 328 wamepatiwa mafunzo ya muda mfupi katika fani tofauti. Pamoja na kuwatambua mafundi wazoefu 224 wa Pemba i na kuingizwa katika mfumo wa vyeti kupitia programu ya Recognition to Prior Learning (RPL).

- vi) Wizara imeendelea kutangaza na kuhamasisha huduma na fursa za Mafunzo ya Amali kupitia vyombo mbalimbali vya habari na maonesho ya kitaifa, ikiwemo Maonesho ya Nane Nane. Jitihada hizo zimehusisha pia utoaji wa matangazo, makala maalumu na utayarishaji wa bango ya matangazo kwa lengo la kuongeza uelewa wa wananchi kuhusu mafunzo hayo.
- vii) Wizara imewawezesha wanafunzi kupata mafunzo ya vitendo katika vyuo vya amali ili kuongeza ujuzi wa kazi na uwezo wa kujitegemea, ambapo zaidi ya wanafunzi 1,136 waliomaliza Kidato cha Pili wamenufaika na mafunzo hayo. Aidha, matumizi ya TEHAMA yameendelea kuimarishwa kupitia uingizaji wa taarifa za wanafunzi 1,861 katika mfumo wa matokeo, maboresho ya mfumo wa taarifa za wafanyakazi (HRMIS), uingizaji wa taarifa za watumishi wapya 53, pamoja na ununuzi wa vifaa vya TEHAMA kwa ajili ya kuongeza ufanisi wa kazi katika ofisi za MMA.

Utekelezaji wa Shabaha

- i) Idadi ya vikundi vya vijana waliojiajiri imeongezeka kutoka 28 mwaka 2024 hadi kufikia 32 mwaka 2026.
- ii) Idadi ya wanafunzi wanaojiunga na Mafunzo ya Amali imeongezeka kutoka wanafunzi 1,803 mwaka 2025 hadi kufikia wanafunzi 2,146 mwaka 2026.
- iii) Jumla ya vijana 720 wamehitimu mafunzo ya amali katika vyuo vya Mamlaka ya Mafunzo ya Amali mwaka 2025/2026.

PROGRAMU YA TANO: UBORA WA ELIMU

32. Mheshimiwa Spika, programu hii ina lengo la kuhakikisha elimu inayotolewa katika ngazote ni yenye ubora unaokidhi mahitaji ya mwenye kuhitimu, jamii na taifa kwa ujumla. Programu hii ilitengewa jumla ya **TSh. 64,540,423,000**, kati ya fedha hizo **TSh. 9,436,126,050** ni kwa ajili ya malipo ya mishahara ya wafanyakazi, **TSh. 11,048,889,950** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo na jumla ya **TSh. 44,055,407,000** zilitengwa kwa shughuli za maendeleo. Hadi kufikia Aprili 2026, jumla ya **TSh. 29,376,573,978** sawa na asilimia 45.5 ya makadirio zilipatikana. Jumla ya **TSh. 7,240,633,192** sawa na asilimia 76.7 ya fedha zilizotengwa kwa ajili ya mishahara zimetumika na **TSh. 7,835,375,433** zimetumika kwa matumizi mengineyo sawa na asilimia 70.9 ya makadirio ya kutekeleza shughuli hizo. Kwa upande wa fedha za maendeleo, jumla ya **TSh. 14,300,565,354** zilipatikana sawa na asilimia 32.5. Kati ya fedha hizo, **TSh. 3,988,551,164** sawa na asilimia 16.1 ya fedha za Serikali kwa shughuli za maendeleo zimepatikana na **TSh. 10,312,014,190** sawa na asilimia 53.5 ya fedha kutoka kwa Washirika wa Maendeleo zilizutumika. Programu hii ina jumla ya programu ndogo tatu na maeneo matano ya kutoa huduma kama ifuatavyo: -

Huduma ya Mitaala na Vifaa vya Kufundishia

33. Mheshimiwa Spika, Huduma hii ina madhumuni ya kutayarisha mitaala ya elimu, kuratibu upatikanaji wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia kwa ngazi za elimu

ya maandalizi, msingi, Sekondari na mafunzo ya Ualimu. Shughuli za utoaji wa huduma hii zinatekelezwa na Taasisi ya Elimu Zanzibar. Kwa mwaka wa fedha 2025/2026, Taasisi ilitengewa ruzuku yenye jumla ya **TSh. 8,331,500,000**. Kati ya fedha hizo **TSh. 515,700,000** ni ruzuku kwa ajili ya matumizi mengineyo, **TSh. 1,590,800,000** ni ruzuku ya malipo ya mishahara ya wafanyakazi na **TSh. 6,225,000,000** ni kwa ajili ya shughuli za maendeleo. Hadi kufikia Aprili 2026, jumla ya **TSh. 7,772,445,537** sawa na asilimia 93.3 ya makadirio zilipatikana. Jumla ya **TSh. 1,213,722,988** sawa na asilimia 76.3 ya fedha zilizotengwa kwa ajili ya mishahara zimetumika na **TSh 136,200,900** zimetumika kwa matumizi mengineyo sawa na asilimia 26.4 ya makadirio ya kutekeleza shughuli hizo. Kwa upande wa fedha za maendeleo, jumla ya **TSh. 6,422,521,649** sawa na asilimia 103.2 zilipatikana. Kati ya fedha hizo, **TSh. 133,955,000** sawa na asilimia 6.7 ya fedha zilizopangwa kwa upande wa Serikali zilipatikana na **TSh. 6,288,566,649** sawa na asilimia 148.8 ya fedha zilizotengwa kwa Washirika wa Maendeleo zimepatikana. Utekelezaji halisi wa huduma hii ni kama ifuatavyo: -

- i) Wizara imeendelea kuimarisha upatikanaji wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia kwa kuchapisha na kusambaza vitabu nakala 145,086 vya Maandalizi Mwaka wa Pili, 138,684 vya Darasa la II na 124,362 vya Darasa la III. Aidha, nakala 30,000 za vitabu vya hadithi zimechapishwa ili kukuza stadi za kusoma, kuandika na kuhesabu. Katika ngazi ya sekondari, nakala 605,953 zimechapishwa na kusambazwa zikiwemo

- 299,702 za Kidato cha Tatu na Nne na 306,251 za fasihi. Vilevile rasimu 16 za vitabu vya darasa la tano na sita na miongozo ya walimu zipo katika hatua ya majaribio kabla ya matumizi rasmi.
- ii) Wizara imeendelea kuwajengea uwezo walimu, wakufunzi wa vyuo vya ualimu na wataalamu wa mitaala katika utekelezaji wa mitaala mbalimbali. Ambapo jumla ya walimu 6,039, wakufunzi 246 na wataalamu wa mitaala 45 walipatiwa mafunzo. Mafunzo hayo yalihusu matumizi ya mitaala, mbinu za ufundishaji na utekelezaji wa mtaala wa umahiri.
 - iii) Wizara imetayarisha na kusambaza moduli 36 za Mtaala wa Stashahada ya Mafunzo ya Ualimu katika fani za Elimu ya Msingi, Elimu Mjumuisho na Elimu ya Maandalizi (ECD), pamoja na kuchapisha mihutasari 14,000 kwa vyuo vya ualimu na vituo vya walimu Unguja na Pemba. Vilevile, miongozo mitano ya kufundishia imeandaliwa kwa wanafunzi wenye mahitaji maalum na masuala ya afya ya uzazi, VVU/UKIMWI, ukatili wa kijinsia na stadi za maisha.
 - iv) Wizara imetayarisha mifumo ya upimaji na tathmini ya kitaifa (National Assessment Framework and Large Scale Assessment) ili kuimarisha utekelezaji wa mtaala. Aidha, inaendelea kuandaa maudhui ya mtaala katika mfumo wa kidijitali kwa lengo la kuboresha upatikanaji wa vifaa na huduma za kufundishia.
 - v) Wizara imefanya mapitio ya Sheria na Muundo wa Taasisi ya Elimu ya Zanzibar Na. 4 ya mwaka 2016 kwa lengo la kuendana na utekelezaji wa mageuzi ya elimu.

Rasimu ya marekebisho kwa sasa ipo katika hatua ya kuwasilishwa kwa mamlaka husika za Serikali kwa ajili ya maamuzi.

Utekelezaji wa Shabaha

- i) Jumla ya miongozo 36 ya kufundishia mafunzo ya ualimu (Training Modules and Manuals) na miongozo Minne ya kufundishia wanafunzi wenye mahitaji maalum imeandaliwa.
- ii) Rasimu za vitabu 16 vya darasa la tano na sita pamoja na viongozi vya walimu zimeandaliwa.
- iii) Jumla ya walimu 3,238 wa madarasa ya kidato cha Pili, Tano na Sita wamepatiwa mafunzo kuhusu mtaala mpya.

Huduma ya Upimaji na Tathmini ya Elimu

34. Mheshimiwa Spika, Programu hii ina madhumuni ya kupima na kutathmini utoaji wa elimu. Shughuli za huduma hii zinatekelezwa na Baraza la Mitihani la Zanzibar. Kwa mwaka wa fedha 2025/2026 huduma ya Upimaji na Tathmini ilitengewa ruzuku ya **Sh. 14,332,500,000**, Kati ya fedha hizo **TSh. 6,907,000,000** ni ruzuku kwa ajili ya matumizi mengineyo, **TSh. 1,425,500,000** ni ruzuku ya malipo ya mishahara ya wafanyakazi na **TSh. 6,000,000,000** ni kwa ajili ya kazi za Maendeleo. Hadi kufikia April 2026, jumla ya **TSh. 7,904,739,225** sawa na asilimia 54.5 zilipatikana. Kati ya fedha hizo **TSh. 1,141,510,925** sawa na asilimia 80.1 zimetumika kulipia mishahara ya wafanyakazi na **Tsh. 6,763,228,300** sawa na asilimia 97.8 zimetumika kwa ajili

ya matumizi mengineyo. Utekelezaji halisi wa shughuli za huduma hii ni kama ifuatavyo:

- i) Wizara imekamilisha uratibu na uendeshaji wa mitihani ya Taifa kwa mwaka 2025 pamoja na kuandaa ripoti, kutangaza matokeo na kufanya mapitio ya miundo ya upimaji na mitihani. Sambamba na hatua hiyo, Wizara imekamilisha malipo ya kazi maalumu kwa walimu walioshiriki kusimamia na kusahihisha mitihani hiyo.
- ii) Wizara imekamilisha utungaji na upitiaji wa maswali pamoja na uendeshaji wa mitihani kwa watahiniwa 1,447 wa vyuo vya ualimu ngazi ya Cheti kwa mwaka 2025. Aidha, imekamilisha uandaaji na uchapaji wa vyeti vya wahitimu wa mafunzo ya ualimu ngazi ya Diploma na Cheti kwa miaka ya 2024 na 2025.
- iii) Wizara imekamilisha zoezi la kuandaa ripoti ya matokeo ya Upimaji wa Darasa la Pili (EGRA & EGMA) kwa mwaka 2025. Jumla ya wanafunzi 3,497 (1,766 W'ke na 1,731 W'me) kutoka skuli 178 za Serikali walishiriki katika upimaji huo ambapo matokeo yanaonesha kuwa kati yao, wanafunzi 1,588 sawa na asilimia 45.4 wamefikia kiwango cha umahiri wa kusoma, kuandika na kuhesabu.
- iv) Wizara imekamilisha mafunzo ya upimaji wa umahiri na English Proficiency Test (EPT) kwa washiriki 44, wakiwemo waratibu wa masomo, watakwimu wa Baraza la Mitihani na maafisa kutoka Taasisi ya Elimu, Mafunzo ya Ualimu na Walimu. Mafunzo hayo yamelenga kuimarisha utekelezaji wa mtaala mpya unaoendana na mageuzi ya elimu.

- v) Wizara imekamilisha maandalizi ya ujenzi wa jengo la Ofisi ya Baraza la Mitihani ikiwemo Uandaaji wa Michoro pamoja na BoQ. Kwa sasa Wizara ipo katika hatua za kumpata Mkandarasi wa ujenzi wa jengo hilo.
- vi) Wizara imekamilisha zoezi la Ukaguzi na Usajili wa vituo vipya 61 vya mitihani vya Skuli za Serikali na Binafsi kwa Skuli za Msingi na Sekondari, Unguja na Pemba. Jumla ya vituo 15 (Serikali vinne na Binafsi 11) vya Sekondari na 46 (Serikali vinne na binafsi 42) vya Msingi vimekaguliwa na kupatiwa nambari za usajili.

Utekelezaji wa Shabaha

- i) Kiwango cha ufaulu kimeendelea kuimarika katika mitihani ya kitaifa katika ngazi mbalimbali. Ufaulu wa Mtihani wa Darasa la Nne umeongezeka kutoka asilimia 93.6 mwaka 2024 hadi asilimia 94.08 mwaka 2025. Vilevile, ufaulu wa Mtihani wa Darasa la Saba umeongezeka kutoka asilimia 96.7 hadi asilimia 99.9, idadi ya wanafunzi waliofaulu kujiunga na vipawa maalum ikiongezeka kutoka 228 hadi 314 na ufaulu wa michepuo kutoka 4,816 hadi 5,975. Aidha, kiwango cha ufaulu katika Mtihani wa Kidato cha Pili kimeongezeka kutoka asilimia 84.44 mwaka 2024 hadi asilimia 93.24 mwaka 2025.
- ii) Kiwango cha ufaulu katika mitihani ya mafunzo ya ualimu kimeendelea kuimarika mwaka 2025. Ambapo wanafunzi 1,371 sawa na asilimia 96.89 walifaulu mtihani wa Cheti cha Ualimu Maandalizi (CECE),

wanafunzi 785 sawa na asilimia 95.6 walifaulu mtihani wa Stashahada ya Msingi, na wanafunzi watatu sawa na asilimia 100 walifaulu mtihani wa Stashahada ya Sekondari.

Huduma ya Ukaguzi wa Elimu

35. Mheshimiwa Spika, huduma hii ina madhumuni ya kusimamia ubora wa elimu inayotolewa kwa kuhakikisha Sera, Sheria, Miongozo na taratibu zilizowekwa na Serikali zinafuatwa. Shughuli za huduma hii zinatekelezwa na Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Elimu. Kwa mwaka wa fedha 2025/2026, huduma hii ilipangiwa jumla ya ruzuku ya **TSh. 3,461,300,000**, Kati ya fedha hizo **TSh. 767,900,000** ni ruzuku kwa ajili ya matumizi mengineyo na **TSh. 2,693,400,000** ni ruzuku ya malipo ya mishahara ya wafanyakazi. Hadi kufikia Aprili 2026, jumla ya **TSh. 2,353,050,510** sawa na asilimia 68.0 zilipatikana. Kati ya fedha hizo **Tsh. 2,147,313,110** sawa na asilimia 79.7 ya fedha zilizotengwa kwa ajili ya mishahara zimetumika na **Tsh. 205,737,400** sawa na asilimia 26.8 zimetumika kwa ajili ya matumizi mengineyo. Utekelezaji wa shughuli za huduma hii ni kama ifuatavyo: -

- i) Wizara imekagua skuli 1,144 kati ya 1,256 zilizopangwa Unguja na Pemba sawa na asilimia 75, zikiwemo 146 za Maandalizi, 503 za Msingi na 295 za Sekondari. Aidha, walimu 3,422 kati ya 4,232 waliopangwa, sawa na asilimia 75, walikaguliwa na kupatiwa ushauri wa kitaaluma ambapo asilimia 76 ya walimu waliofuatiliwa walijirekebisha.

- ii) Wizara imeimarisha mfumo wa ukaguzi kwa kufanya mapitio ya zana ya ukaguzi wa vyuo vya ualimu na kuwapatia mafunzo wakaguzi wa elimu na wakaguzi wa ndani wa skuli 1,538 kuhusu matumizi ya Mfumo wa Taarifa za Ukaguzi wa Skuli. Ufuatiliaji katika skuli 18 za Unguja umeonesha kuwa asilimia 95 ya wakaguzi wanafuata sheria na miongozo ya ukaguzi.
- iii) Katika kuimarisha uwezo wa kitaaluma, walimu 192 wamepatiwa mafunzo ya uandaaji wa maswali ya mitihani na uchambuzi wa matokeo ya wanafunzi. Aidha, wakaguzi na watumishi 125 walipatiwa mafunzo ya elimu mjumuisho na elimu kwa wenye mahitaji maalum.
- iv) Wizara imeendelea kuwajengea uwezo watendaji wake, ambapo watendaji wawili wanaendelea na mafunzo ya muda mrefu katika Chuo Kikuu cha Zanzibar na ICPS sambamba na hilo, mtendaji mmoja alipatiwa mafunzo ya muda mfupi kuhusu mfumo wa kimataifa wa ufungaji wa hesabu wa sekta ya umma (IPSAS).

Utekelezaji wa Shabaha

- i) Idadi ya skuli zilizokaguliwa imeongezeka kutoka skuli 921 mwaka 2024/2025 na kufikia skuli 1,144 kwa mwaka 2025/2026 sawa na asilimia 75 ya shabaha.
- ii) Idadi ya walimu waliokaguliwa imeongezeka kutoka walimu 2,911 kwa mwaka 2024/2025 hadi kufikia walimu 3,422 kwa mwaka 2025/2026 sawa na asilimia 75 ya shabaha.

Huduma za Maktaba

36. Mheshimiwa Spika, Programu hii ina madhumuni ya kuimarisha usomaji kwa kutoa fursa ya kutumia vitabu, nyaraka na nyenzo nyengine za taaluma kwa watoto, wanafunzi wa ngazi zote na jamii. Shughuli za huduma hii zinatekelezwa na Bodi ya Huduma za Maktaba Zanzibar. Kwa mwaka wa fedha 2025/2026 huduma hii ilipangiwa kutumia ruzuku ya **TSh. 5,921,400,000**, Kati ya fedha hizo **TSh. 1,087,300,000** ni ruzuku kwa ajili ya matumizi mengineyo na **TSh. 1,134,100,000** ni ruzuku ya malipo ya mishahara ya wafanyakazi na **TSh. 3,700,000,000** ni kwa ajili ya maendeleo. Hadi kufikia Aprili, 2026 jumla ya **TSh 1,391,604,408** sawa na asilimia 23.5 zilipatikana. Kati ya fedha hizo **TSh. 860,106,838** sawa na asilimia 75.8 zimetumika kulipia mishahara ya wafanyakazi na **TSh. 360,824,010** sawa na asilimia 33.2 zimetumika kwa ajili ya matumizi mengineyo na **TSh 170,673,560** sawa na asilimia 5.3 ya fedha zilizotengwa kwa upande wa Serikali kwa ajili ya shughuli za maendeleo zimepatikana. Utekelezaji halisi wa shughuli za huduma hii ni kama ifuatavyo:

- i) Wizara imeendelea kuhamasisha wanafunzi na jamii juu ya utamaduni wa kujisomea pamoja na matumizi ya maktaba ambapo watumiaji wamafikia 54,752 ikilinganishwa na 48,797 mwaka 2024, na wanachama 1,068 walisajiliwa. Aidha, programu 379 ziliendeshwa, zikiwemo 46 za vijana, 64 za nje ya maktaba, 84 za watoto na 185 za ziara za kimasomo.

- ii) Wizara imefanikiwa kupata jumla ya vitabu 36,866 vikiwemo 15,407 vilivyounuliwa na Serikali, 20,266 kutoka Book Aid International, 298 kutoka kwa wadau wengine na 895 vya mtaala mpya kutoka Taasisi ya Elimu Zanzibar. Aidha, machapisho 1,221 yakiwemo magazeti yamenunuliwa kwa ajili ya kuwapatia wananchi taarifa na maarifa.
- iii) Wizara imeendelea kuimarisha miundombinu ya maktaba ambapo ukarabati wa jengo la zamani la Maktaba Kuu tawi la Pemba lililopo Chachani, Chake Chake umefikia asilimia 95. Kwa upande wa Unguja, hatua za awali za upembuzi yakinifu, usanifu wa michoro, uchunguzi wa ardhi na makadirio ya gharama za ujenzi wa Maktaba Kuu ya Zanzibar zimekamilika.
- iv) Wizara imeimarisha huduma za maktaba kwa kuanzisha na kuboresha maktaba 34 Unguja na Pemba, zikiwemo 13 za sekondari, 9 za msingi, 10 za maandalizi, moja ya Chuo cha Ualimu Nkrumah na moja ya Chuo cha Mafunzo Zanzibar kilichopo Kiinua Miguu.
- v) Wizara imeendelea kuwajengea uwezo watumishi wa maktaba, ambapo watumishi 2 wamepatiwa mafunzo ya muda mrefu na baadhi ya wafanyakazi wamepatiwa mafunzo ya muda mfupi katika maeneo ya afya ya akili, huduma kwa wateja, mapambano dhidi ya rushwa, usalama wa mtandao, utunzaji kumbukumbu, mifumo ya TEHAMA, bajeti na ukutubi.
- vi) Katika kutangaza huduma za maktaba, Wizara imeshiriki katika maonesho na maadhimisho mbalimbali ya kitaifa, jambo lililoweza wageni 2,851 kutembelea banda

la huduma za maktaba na kupata taarifa, elimu na machapisho mbalimbali.

Utekelezaji wa Shabaha

- i) Idadi ya wanachama waliosajiliwa imeongezeka kutoka 643 mwaka 2024/2025 hadi kufikia wanachama 1,068 mwaka 2025/2026.
- ii) Idadi ya watumiaji wa maktaba imeongezeka kutoka 48,601 mwaka 2024/2025 hadi kufikia watumiaji 54,752 mwaka 2025/2026.
- iii) Idadi ya maktaba zilizoimarishwa imeongezeka kutoka 19 mwaka 2024/2025 hadi kufikia 34 mwaka 2025/2026.
- iv) Taratibu za Ujenzi wa jengo jipya la Maktaba kuu ya Taifa zinaendelea ambapo michoro imekamilika na kwa sasa Wizara inaendelea na mazungumzo na wawekezaji kwa ajili ya utekelezaji wa Mradi huu.

Huduma ya Baraza la Elimu

37. Mheshimiwa Spika, huduma hii ina madhumuni ya kuhakikisha Sheria, Sera na Taratibu zilizowekwa na Serikali zinafuatwa katika uendeshaji wa skuli za Serikali na za binafsi. Huduma hii pia inatoa leseni kwa walimu na kuzisajili skuli za Serikali na za binafsi pamoja na vyuo vya ualimu vya kati. Kwa mwaka wa fedha 2025/2026, huduma hii ilipangiwa kutumia jumla ya ruzuku ya **TSh. 718,300,000**, Kati ya fedha hizo **TSh. 352,500,000** ni ruzuku kwa ajili ya matumizi mengineyo na **TSh. 365,800,000** ni ruzuku ya malipo ya mishahara ya wafanyakazi. Hadi kufikia

Aprili 2026, jumla ya **TSh. 359,348,658** sawa na asilimia 50.0 zilipatikana. Kati ya fedha hizo **TSh. 290,814,600** sawa na asilimia 79.5 zimetumika kulipia mishahara ya wafanyakazi na **TSh. 68,534,058** sawa na asilimia 19.4 ya fedha zilizopangwa kwa matumizi mengineyo zimetumika. Utekelezaji halisi wa huduma hii ni kama ifuatavyo: -

- i) Wizara imeendelea kuimarisha usimamizi wa walimu kwa kutoa leseni 10,500 za kielektroniki wakiwemo walimu wa Maandalizi (2,306), Msingi (3,549) na Sekondari (4,645), pamoja na leseni 82 za karatasi.
- ii) Wizara imefanya uhakiki wa skuli 1,522 za Serikali na Binafsi na kusajili skuli 1,426 katika ngazi mbalimbali za elimu, zikiwemo skuli 15 mpya na 1,411 zilizoongeza muda wa usajili..
- iii) Wizara imefanya vikao viwili na Walimu Wakuu wa skuli za Serikali na Binafsi pamoja na wadau wa elimu katika Wilaya zote za Unguja kwa lengo la kutatua changamoto na kuimarisha utoaji wa huduma za elimu. Aidha, kesi 72 za udhalilishaji ziliripotiwa zikiwemo 44 za ujauzito, 13 za kubakwa, saba za kulawitiwa na sita za kutoroshwa

Utekelezaji wa Shabaha

- i) Idadi ya leseni za walimu zimeongezeka kutoka leseni 6,105 kwa mwaka 2024/2025 hadi kufikia leseni 10,500 kwa mwaka 2025/2026.
- ii) Jumla ya skuli mpya 32 zimesajiliwa mwaka 2025/2026.

Programu ndogo ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano katika Elimu

38. Mheshimiwa Spika, Programu hii ina madhumuni ya kuifanya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano itumike katika ngazi ya utawala, kujifunza na kufundishia, kuimarisha huduma ya mawasiliano na kutunza usalama wa taarifa. Shughuli za programu hii zinatekelezwa na Idara ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano katika Elimu. Kwa mwaka wa fedha 2025/2026, programu hii ilipangiwa kutumia jumla ya **TSh. 26,368,829,000**, Kati ya fedha hizo, **TSh. 547,160,550** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo na **TSh. 591,261,450** ni kwa malipo ya mishahara na **TSh. 25,230,407,000** ni kwa ajili ya shughuli za maendeleo, kati ya fedha hizo **TSh 10,695,000,000** ni kutoka SMZ na **TSh 14,535,407,000** ni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo. Hadi kufikia April 2026, jumla ya **TSh. 8,131,102,947** sawa na asilimia 30.8 zilipatikana. Kati ya fedha hizo **TSh. 578,800,733** sawa na asilimia 97.9 ya fedha zilizopangwa kwa ajili ya mishahara ya zimetumika na **Tsh. 78,018,069** sawa na asilimia 14.3 ya fedha za matumizi mengineyo zimepatikana. Kwa upande wa fedha za maendeleo, jumla ya **TSh. 7,474,284,145** sawa na asilimia 29.6 zilipatikana. Kati ya fedha hizo, **TSh. 3,450,836,604** sawa na asilimia 32.3 ya fedha zilizopangwa kwa upande wa Serikali zilipatikana na **TSh. 4,023,447,541** sawa na asilimia 27.7 ya fedha zilizotengwa kwa Washirika wa Maendeleo zimepatikana. Utekelezaji halisi wa programu hii ni kama ifuatavyo: -

- i) Wizara imeimarisha mazingira ya kidijitali katika skuli kwa kuanzisha maabara 19 za kompyuta, vyumba 33 vya e-Library, madarasa janja 20 pamoja na kununua desktop 2,000, laptop 858 na smartboards 40. Aidha, site 74 zikiwemo skuli 66 na taasisi nane za elimu zimeunganishwa na mkonga wa mawasiliano.
- ii) Katika kujenga uwezo wa matumizi ya TEHAMA, watendaji 10 wamepatiwa mafunzo ya usimamizi wa LMS, wakufunzi mahiri 50 wamejengewa uwezo na walimu 1,389 wamepatiwa mafunzo ya digital literacy kwa ajili ya kufundishia kwa kutumia teknolojia.
- iii) Wizara imeimarisha mtandao wa ndani (LAN) katika Ofisi Kuu ya Wizara Mazizini Unguja sambamba na usimikaji wa kamera 57 za CCTV na kifaa cha kurekodi (NVR) kwa ajili ya kuimarisha usalama wa mifumo ya TEHAMA.
- iv) Wizara imeendelea kuimarisha utoaji wa maudhui ya elimu kwa kuandaa makala 11 za televisheni na 31 za redio, vipindi viwili vya TV, vipindi 50 vya redio katika masomo mbalimbali. Vilevile, imefanya matengenezo ya vifaa vya TEHAMA na mifumo ya utangazaji pamoja na kutatua hitilafu ya transmita ya Elimu FM katika kituo cha Masingini.

Utekelezaji wa Shabaha

- i) Idadi ya walimu waliopata mafunzo ya TEHAMA kwa mwaka imeongezeka kutoka walimu 817 mwaka 2024/2025 hadi kufikia walimu 1,389 mwaka 2025/2026.

- ii) Idadi ya skuli zilizounganishwa na mkonga wa taifa zimeongezeka kutoka skuli 70 za Sekondari mwaka 2024/2025 hadi kufikia Skuli 140 mwaka 2025/2026.
- iii) Jumla ya Skuli 314 zimemepatiwa vifaa vya Teknolojia ya Habari na mawasiliano.
- iv) Skuli zinazotumia TEHAMA katika ufundishaji zimeongezeka kutoka skuli 227 mwaka 2024/2025 hadi skuli 563 mwaka 2025/2026.

Programu ndogo ya Elimu Mjumuisho na Stadi za Maisha

39. Mheshimiwa Spika, Programu hii ina jukumu la kuhakikisha upatikanaji wa elimu kwa watoto wote wakiwemo wenye mahitaji maalum. Programu hii inatekelezwa na Kitengo cha Elimu Mjumuisho na Stadi za Maisha. Kwa mwaka wa fedha 2025/2026, programu hii ilitengewa jumla ya **TSh. 200,000,000** kwa matumizi mengineyo. Hadi kufikia Aprili, 2025, jumla ya **TSh. 14,870,000** sawa na asilimia 7.4 zilipatikana. Utekelezaji halisi wa shughuli za programu hii ndogo ni kama ifuatavyo: -

- i) Wizara imeendelea kuimarisha utekelezaji wa Elimu Mjumuisho na Stadi za Maisha kwa kufanya ufuatiliaji katika skuli 73, zikiwemo 54 za msingi na 19 za sekondari, pamoja na kufanya mkutano wa maafisa na washauri 20 kuhusu ukusanyaji wa taarifa za wanafunzi wenye ulemavu.
- ii) Katika kuimarisha utambuzi na huduma kwa wanafunzi wenye mahitaji maalum, Wizara imetoa mafunzo kwa

wajumbe 120 wa timu za wataalamu kuhusu matumizi ya vifaa vya upimaji kabla ya watoto kuanza skuli, kufanya upimaji wa majaribio kwa watoto 1,742 katika skuli 18 na kupima wanafunzi 209 wenye changamoto za uoni. Aidha, wanafunzi 1,070 walifanyiwa uchunguzi wa uoni ambapo 167 walibainika na changamoto na kupatiwa miwani sambamba na ugawaji wa aina 13 za vifaa saidizi kwa wanafunzi wenye ulemavu katika skuli za Unguja na Pemba.

- iii) Wizara imeendelea kujenga uwezo wa walimu na wadau kwa kutoa mafunzo kwa washiriki 406 kuhusu muongozo wa klabu za skuli na stadi za maisha, walimu 200 wa ushauri na unasihi kuhusu stadi za maisha, walimu 129 wa Madrasat Al-Ahbaab kuhusu nidhamu endelevu, pamoja na wauzaji wa vyakula wa skuli 124 na walimu 115 wa lishe na mazingira kuhusu lishe bora.
- iv) Katika kuimarisha maadili na ulinzi wa watoto, Wizara imewajengea uwezo wanafunzi 906 kuhusu udhalilishaji wa kijinsia, kufanya kongamano kwa walimu 52 wa dini kuhusu maadili na uadilifu pamoja na kongamano la walimu wakuu na maafisa 118 kuhusu udhibiti wa matumizi ya dawa za kulevya miongoni mwa wanafunzi.
- v) Aidha, Wizara kwa kushirikiana na NAD imefanya utafiti kuhusu programu ya Home Based Schooling kwa lengo la kubaini watoto wasioweza kuhudhuria skuli na kuweka msingi wa maamuzi ya kuanzisha utaratibu huo, ambapo kwa sasa utafiti huo upo katika hatua ya uandishi wa ripoti.

Utekelezaji wa Shabaha

- i) Idadi ya walimu waliopatiwa mafunzo ya elimu mjumuisho na stadi za maisha imeongezeka kutoka 1,066 mwaka 2024/2025 hadi 2,096 mwaka 2025/2026.
- ii) Idadi ya wanafunzi walioandikishwa wenye mahitaji maalumu imeongezeka kutoka 10,269 mwaka 2024/2025 hadi kufikia wanafunzi 10,341mwaka 2025/2026.

Programu ndogo ya Michezo na Utamaduni

40. Mheshimiwa Spika, Programu hii ina madhumuni ya kumuandaa mwanafunzi kimwili, kiafya na kiakili katika kujifunza kwa kupitia michezo. Shughuli za programu hii zinatekelezwa na Idara ya Michezo na Utamaduni katika elimu. Kwa mwaka wa fedha 2025/2026, programu hii ilipangiwa kutumia jumla ya **TSh. 5,206,594,000**. Kati ya fedha hizo, **TSh. 671,329,400** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo na **TSh. 1,635,264,600** ni kwa matumizi ya mishahara na **TSh. 2,900,000,000** ni kwa ajili ya maendeleo. Hadi kufikia Aprili, 2026, jumla ya **TSh. 1,449,412,694** sawa na asilimia 27.8 zilipatikana. Kati ya fedha hizo **TSh. 1,008,363,998** sawa na asilimia 61.7 ya fedha zilizotengwa kwa ajili ya mishahara zimetumika na **TSh. 207,962,696** sawa na asilimia 31.0 ya fedha za matumizi mengineyo zimetumika na **TSh 233,086,000** sawa na asilimia 8.0 ya fedha zilizotengwa kwa ajili ya shughuli za maendeleo zimepatikana kutoka SMZ. Utekelezaji wa programu hii ni kama ifuatavyo: -

- i) Wizara imeendelea kuimarisha michezo na utamaduni katika skuli kwa kuwapatia mafunzo walimu 849 wa michezo, utamaduni na skauti kutoka Wilaya zote za Unguja na Pemba pamoja na kutoa mafunzo ya usalama majini na uokozi kwa walimu 1,636 na wanafunzi 82,988 kwa kushirikiana na The Panje Project.
- ii) Katika kuimarisha usimamizi na ushiriki wa wanafunzi, Wizara imefanya ufuatiliaji wa shughuli za skauti katika skuli 45 na michezo pamoja na sanaa katika skuli 105 za Serikali na Binafsi kwa lengo la kukuza maadili, afya na vipaji vya wanafunzi. Aidha, skuli 143 zimepatiwa vifaa vya michezo.
- iii) Wizara imeendelea kukuza vipaji vya wanafunzi kupitia mashindano na majukwaa mbalimbali, ikiwemo Kongamano la Kitaifa la Michezo na Utamaduni lililowashirikisha washiriki 250, mashindano ya sanaa kwa wanafunzi 66 wenye mahitaji maalum na mashindano ya MABUME yaliyowahusisha wanafunzi 600 wa Unguja na Pemba.
- iv) Wizara imekamilisha hatua za maandalizi ya viwanja vya michezo ikiwemo uandaaji wa michoro na BOQ.

Utekelezaji wa Shabaha

- i) Idadi ya walimu waliopatiwa taaluma ya michezo na utamaduni imeongezeka kutoka walimu 500 mwaka 2024/2025 hadi kufikia walimu 1,349 mwaka 2025/2026.
- ii) Skuli zilizopatiwa vifaa vya michezo zimeongezeka kutoka skuli 30 mwaka 2024/2025 hadi kufikia skuli 143 kwa mwaka 2025/2026.

PROGRAMU YA SITA: UTAWALA NA UONGOZI

41. Mheshimiwa Spika, Programu ya Utawala na Uongozi ina lengo la kuhakikisha usimamizi wa matumizi na upatikanaji wa rasilimali bora katika utekelezaji wa Mipango ya Maendeleo ya elimu. Programu hii ina programu ndogo tatu zikiwemo Programu ndogo ya Uongozi kwa Ujumla, Programu ndogo ya shughuli za Mipango, Sera na Utafiti na Programu ndogo ya uratibu wa shughuli za Elimu Pemba. Programu hii ilipangiwa jumla ya **TSh. 49,015,520,000**, kati ya fedha hizo **TSh. 10,062,235,250** ni kwa ajili ya malipo ya mishahara ya wafanyakazi, TSh. 14,903,284,750 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo na jumla ya **TSh. 24,050,000,000** zilitengwa kwa shughuli za maendeleo, kati ya fedha hizo **TSh 11,050,000,000** ni kutoka SMZ na **TSh 13,000,000,000** ni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo. Hadi kufikia Aprili 2026, jumla ya **TSh. 26,520,409,055** sawa na asilimia 54.1 ya makadirio zilipatikana. Jumla ya **TSh. 9,579,623,621** sawa na asilimia 95.2 ya fedha zilizotengwa kwa ajili ya mishahara zimetumika na **TSh 9,819,188,161** zimetumika kwa matumizi mengineyo sawa na asilimia 65.9 ya makadirio ya kutekeleza shughuli hizo. Kwa upande wa fedha za maendeleo, jumla ya **TSh. 7,121,597,273** zilipatikana sawa na asilimia 29.6. Kati ya fedha hizo, **TSh. 2,996,261,643** sawa na asilimia 27.1 ya fedha zilizotengwa kwa upande wa Serikali zimepatikana na **TSh. 4,125,335,630** sawa na asilimia 31.7 ya fedha za Washirika wa Maendeleo zimetumika. Utekelezaji halisi wa programu hii ni kama ifuatavyo:

Programu ndogo ya Uongozi kwa Ujumla

42. Mheshimiwa Spika, programu hii ina madhumuni ya kuhakikisha ufanisi wa Uongozi na Utawala wa rasilimali za Wizara. Shughuli za programu hii ndogo zinatekelezwa na Idara ya Utumishi na Uendeshaji. Kwa mwaka wa fedha 2025/2026, programu hii ilipangiwa jumla ya **TSh. 31,143,255,000**. Kati ya fedha hizo, **TSh. 9,268,228,000** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo, **TSh. 7,825,027,000** ni kwa matumizi ya mishahara na **TSh. 14,050,000,000** ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo, kati ya fedha hizo **TSh 1,050,000,000** ni kutoka SMZ na **TSh 13,000,000,000** ni kutoka kwa Washirik awa Maendeleo. Hadi kufikia Aprili 2026, jumla ya **TSh. 21,009,932,424** sawa na asilimia 67.5 ya makadirio zilipatikana. Jumla ya **TSh. 7,586,960,798** sawa na asilimia 97.0 ya fedha zilizotengwa kwa ajili ya mishahara zimetumika na **TSh 7,478,156,666** zimetumika kwa matumizi mengineyo sawa na asilimia 80.7 ya makadirio ya kutekeleza shughuli hizo. Kwa upande wa fedha za maendeleo, jumla ya **TSh. 5,944,814,960** sawa na asilimia 42.3 zilipatikana. Kati ya fedha hizo, **TSh. 1,819,479,330** sawa na asilimia 173.3 ya fedha zilizopangwa kwa upande wa Serikali zilipatikana na **TSh. 4,125,335,630** sawa na asilimia 31.7 ya fedha zilizotengwa kwa Washirika wa Maendeleo zimepatikana. Utekelezaji wa kazi za programu hii ni kama ifuatavyo: -

- i) Wizara imeendelea kuimarisha rasilimali watu kwa kuajiri walimu 490 (Unguja 295 na Pemba 195) na kuwapatia mafunzo elekezi (induction course) waajiriwa

wapya 1,461 (Unguja 1,093 na Pemba 368). Aidha, maafisa 10 wamepatiwa mafunzo ya muda mfupi na maafisa watatu mafunzo ya muda mrefu kwa lengo la kuongeza ufanisi wa kazi.

- ii) Wizara imeendelea kuboresha ustawi wa watumishi kwa kulipa mishahara na stahiki mbalimbali, ikiwemo posho za likizo kwa watumishi 1,760 (Unguja 1,490 na Pemba 270), gharama za mazishi kwa wafanyakazi 12 (sita kwa Unguja na sita Pemba) na gharama za ubani kwa wafanyakazi 24 wa Pemba.
- iii) Wizara imeimarisha uendeshaji wa Ofisi za Elimu za Mikoa Unguja na Pemba kwa kuzipatia fedha za uendeshaji pamoja na kuendelea na ujenzi wa Makao Makuu ya Wizara Unguja uliyoufikia asilimia 49 na Ofisi ya Elimu Pemba iliyofikia asilimia 80.
- iv) Wizara imeendelea na mapitio ya Sheria ya Elimu ya mwaka 1982 na kuandaa rasimu ya sheria mpya ya elimu ambayo tayari imewasilishwa kwa wadau mbalimbali wa elimu.

Utekelezaji wa Shabaha

- i) Idadi ya wafanyakazi imeongezeka kutoka 20,514 mwaka 2024/2025 na kufikia 22,514 mwaka 2025/2026.
- ii) Rasimu ya Sheria mpya ya elimu imeandaliwa na imewasilishwa katika ngazi ya Uongozi wa Wizara.
- iii) Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali na Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia wamefanya kikao cha pamoja kwa lengo la kuimarisha mashirikano, kujadili changamoto za Sekta ya Elimu na kuzitafutia utatuzi wake.

Programu ndogo ya Mipango, Sera na Utafiti

43. Mheshimiwa Spika, Madhumuni makubwa ya Programu hii ni kufanikisha na kuratibu utekelezaji wa Mipango, Sera na Utafiti ya Wizara. Programu hii ndogo inatekelezwa na Idara ya Mipango, Sera na Utafiti. Kwa mwaka wa fedha 2025/2026, programu hii ilipangiwa kutumia jumla ya **TSh. 16,103,100,000**. Kati ya fedha hizo, **TSh. 5,065,897,200** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo na **TSh. 1,037,202,800** ni kwa matumizi ya mishahara na **TSh. 10,000,000,000** ni kwa ajili ya shughuli za maendeleo. Hadi kufikia Aprili 2026, jumla ya **TSh. 4,254,232,606** sawa na asilimia 24.6 ya makadirio zilipatikana. Jumla ya **TSh. 894,418,798** sawa na asilimia 86.2 ya fedha zilizotengwa kwa ajili ya mishahara zimetumika na **TSh 2,183,031,495** zimetumika kwa matumizi mengineyo sawa na asilimia 63.1 ya makadirio ya kutekeleza shughuli hizo. Kwa upande wa fedha za maendeleo, jumla ya **TSh. 1,176,782,313** zilipatikana kutoka Serikalini sawa na asilimia 11.8 ya fedha zilizotengwa kwa shughuli za maendeleo. Utekelezaji halisi wa programu hii ni kama hivi ifuatavyo: -

- i) Wizara imeendelea kuimarisha mifumo ya taarifa na takwimu kwa kufanya uhakiki wa taarifa za skuli 664 za Serikali za Unguja na Pemba kupitia Mfumo wa Ukusanyaji wa Taarifa za Skuli (SIS), zikiwemo skuli 84 za Maandalizi, 345 za Msingi, sita za Msingi na Kati, na 229 za Sekondari. Aidha, Wizara imeandaa Muhutasari wa Takwimu za Elimu (Education Statistical Abstract) kwa mwaka 2025 ambao unapatikana katika tovuti ya Wizara.

- ii) Katika kuimarisha mfumo wa sera na tafiti za sekta, Wizara imekamilisha uandaaji wa Sera ya Elimu na sasa ipo katika hatua ya kuwasilishwa kwa Makatibu Wakuu. Aidha, Wizara imekamilisha ripoti ya utafiti wa SEACMEQ V kuhusu uwezo wa wanafunzi wa Darasa la Sita katika kusoma na hisabati
- iii) Wizara imeendelea kusimamia na kufuatilia utekelezaji wa miradi ya elimu ambapo jumla ya miradi 31 ya maendeleo imefanyiwa ufuatiliaji ili kubaini maendeleo ya utekelezaji wake.
- iv) Katika kuimarisha mazingira ya kujifunzia, Wizara imepokea jumla ya kontena 74 zenye vifaa mbalimbali vya elimu, vikiwemo seti za vikatio vya wanafunzi wa msingi na sekondari, vitanda vya wanafunzi wa dakhalia, pamoja na viti na meza za walimu. Aidha, katika maadhimisho ya miaka 62 ya Mapinduzi ya Zanzibar, Wizara imefanikiwa kufungua miradi 39 Unguja na Pemba, ikiwemo skuli 13 za Maandalizi, saba za Msingi na 13 za Sekondari pamoja na kuweka mawe ya msingi katika miradi miwili.
- v) Wizara imeendelea kuimarisha ushirikiano wa sekta kwa kushiriki vikao saba vya mashirikiano na wadau wa maendeleo katika elimu. Aidha, imefanya Mkutano Mkuu wa Tisa wa Tathmini ya Sekta ya Elimu Zanzibar uliowashirikisha wadau wa elimu 170 wakiwemo Washirika wa Maendeleo kwa lengo la kujadili mafanikio, changamoto na maazimio ya kuimarisha stadi za kusoma, kuandika na kuhesabu.

vi) Katika kuwajengea uwezo watumishi wake, Wizara imewapatia mafunzo ya muda mfupi maafisa 12 juu ya matumizi ya Microsoft Power BI programu inayosaidia kuchambua na kuonesha taarifa kwa chati zinazoeleweka kwa urahisi zaidi, upangaji wa miradi, ufuatiliaji na tathmini, pamoja na usimamizi wa fedha. Aidha, mfanyakazi mmoja amepata mafunzo ya muda mrefu katika ngazi ya Shahada ya Uzamili ya fani ya Usimamizi na Upangaji wa Miradi.

Utekelezaji wa Shabaha

- i) Ripoti za utekelezaji na tathmini ya maendeleo ya elimu zimeandaliwa.
- ii) Mapendekezo ya miradi mipya miwili imeandaliwa na kuwasilishwa kwa washirika wa maendeleo kwa ajili ya kupatiwa ufadhili.
- iii) Ripoti ya utafiti wa masuala ya kijisia imekamilika.
- iv) Rasimu ya Sera mpya ya elimu imekamilika na sasa ipo katika hatua za kuidhinishwa na Serikali.
- v) Vikao vitatu baina ya Wizara na Kamati ya Ustawi wa Jamii ya Baraza la Wawakilishi vimefanyika.

Programu ndogo ya Uratibu shughuli za elimu Pemba

44. Mheshimiwa Spika, Programu hii ndogo ina madhumuni ya kuratibu na kusimamia shughuli zote za elimu kwa upande wa Pemba. Msimamizi Mkuu wa shughuli za programu hii ni Afisa Mdhamini wa Elimu Pemba. Programu hii ndogo ilipangiwa jumla ya **TSh. 1,769,165,000**. Kati ya fedha hizo, **TSh. 569,159,550** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo na

Tsh. 1,200,005,450 ni kwa ajili ya matumizi ya mishahara. Hadi kufikia Aprili 2026, jumla ya **Tsh. 1,256,244,025** sawa na asilimia 71.0 zilipatikana. Kati ya fedha hizo **Tsh. 1,098,244,025** sawa na asilimia 91.5 zimetumika kulipia mishahara ya wafanyakazi na **Tsh. 158,000,000** sawa na asilimia 27.8 zimetumika kwa ajili ya matumizi mengineyo. Utekelezaji halisi ni kama ifuatavyo:

- i) Wizara imeimarisha uratibu wa shughuli zake kwa kufanya mikutano katika ngazi ya skuli, Wilaya na Mkoa iliyowashirikisha walimu, wazazi na kamati za skuli kwa lengo la kujadili maendeleo ya wanafunzi na kuongeza ufaulu. Aidha, vikao vya watendaji wakuu na viongozi wa idara na vitengo vimefanyika kwa ajili ya kujadili utendaji kazi, kuimarisha ufuatiliaji na kutatua changamoto zinazojitokeza.
- ii) Wizara imeendelea kufuatilia utekelezaji wa miradi ya maendeleo katika maeneo mbalimbali, ikiwemo ziara za viongozi wa juu wa Serikali katika kutembelea miradi hiyo. Aidha, ufuatiliaji umehusisha pia maendeleo ya ujenzi wa jengo la Ofisi ya Wizara Pemba, ambalo limefikia asilimia 80.
- iii) Wizara imeendelea kusimamia shughuli za elimu katika skuli na maeneo mbalimbali kwa kufanya ziara za ukaguzi wa utekelezaji wa kazi za kila siku, mazingira ya kujifunzia na uendeshaji wa mitihani ya Taifa. Vilevile, katika kuimarisha miundombinu ya elimu, Wizara imefanya ukarabati na ukamilishaji wa majengo mbalimbali, ikiwemo ghala la Ofisi Kuu, nyumba ya

walimu Michakaini, madarasa, ofisi na vyoo katika skuli tofauti.

UTEKELEZAJI WA VIPAUMBELE KWA MUJIBU WA MPANGO MKAKATI WA WIZARA NA TAASISI KWA MWAKA 2025/2026.

45. Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Spika, Utekelezaji halisi wa vipaumbele vya mwaka wa fedha 2025/26 ni kama ifuatavyo:-

- i) Wizara imefanya mikutano 18 ya uhamasishaji wa uandikishaji kwa wanafunzi wa maandalizi na darasa la kwanza iliyowashirikisha washiriki 13,322 kupitia jamii, viongozi na vyombo vya habari 7. Aidha, jumla ya wanafunzi 107,819 wameandikishwa katika ngazi ya maandalizi, 418,959 Msingi na 164,127 sekondari kwa skuli za Serikali na Binafsi.
- ii) Wizara imeanza ujenzi wa skuli 8 za msingi za ghorofa zenye madarasa 256 pamoja na skuli 7 za sekondari zenye madarasa 179 Unguja na Pemba kwa lengo la kuondoa shifti na kupunguza msongamano.
- iii) Kupitia mradi wa HEET unaofadhiliwa na Benki ya Dunia, ujenzi wa maabara ya sayansi umefikia asilimia 67.4 na Skuli ya Kilimo asilimia 78.7, sawa na wastani wa asilimia 73 ya utekelezaji. Aidha, maandalizi ya ujenzi wa majengo ya SUZA kupitia ufadhili wa BADEA.
- iv) Wizara imeanzisha maabara 19 za kompyuta, kuunganisha mkonga katika maeneo 74, kuanzisha madarasa janja 20 na vyumba 33 vya e-Library. Aidha, Wizara imesambaza vifaa vya TEHAMA vikiwemo laptop 858, desktop 2,000 na smartboards 40.

- v) Jumla ya walimu 6,039 kutoka skuli za Serikali na Binafsi wamepatiwa mafunzo ya utekelezaji wa mitaala mbalimbali. Aidha, wakufunzi 246 wa vyuo vya ualimu pamoja na Wakuza Mitaala 45 na wajumbe wa Bodi ya Ushauri walipatiwa mafunzo ya mtaala wa umahiri (CBC). Aidha, Wizara imechapisha na kusambaza nakala za vitabu 145,086 vya Maandalizi Mwaka wa Pili, 138,684 vya Darasa la II na 124,362 vya Darasa la III. Katika ngazi ya sekondari, vitabu 605,953 vimechapishwa na kusambazwa, vikiwemo 299,702 vya Kidato cha Tatu na Nne na 306,251 vya fasihi.
- vi) Wizara imetiliana Saini mkataba wa ununuzi na usambazaji wa vifaa vya mkondo wa amali kwa skuli za Sekondari. Aidha, uandaaji wa michoro ya karakana kwa skuli za Sekondari umekamilika na kwa sasa hatua za kuwapata wakandarasi zinaendelea. Sambamba na hayo, mchakato wa manunuzi wa kuwapata wakandarasi kwa ajili ya ujenzi wa chuo cha mafunzo ya Amali Bweleo na Chambani unaendelea.
- vii) Wizara inaendelea na maandalizi ya ujenzi wa viwanja 3 vya michezo vya skuli za Fidel Castro, Paje Mtule na Mambosasa ambapo hatua ya michoro na BoQ imekamilika kwa sasa taratibu za kumpata mkandarasi zinaendelea. Aidha, jumla ya skuli 143 zimepatiwa vifaa mbalimbali vya michezo.
- viii) Wizara imewapatia mikopo wanafunzi 8,975 wapya, wakiwemo wanaume 3,595 na wanawake 5,362, katika vyuo vya ndani na nje ya Tanzania. Kati yao, 3,640 ni wa

Stashahada, 5,072 Shahada, 227 Shahada ya Uzamili na 18 Shahada ya Uzamivu, sawa na asilimia 183 ya shabaha iliyopangwa.

MWELEKEO WA UTEKELEZAJI WA VIPAUMBELE VYA MATUMIZI KWA WIZARA NA TAASISI ZINAZOSIMAMIWA NA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027.

46. Mheshimiwa Spika, Baada ya kueleza Utekelezaji wa Bajeti kwa Taasisi zinazosimamiwa na Wizara, sasa naomba kuwasilisha mwelekeo wa Utekelezaji wa Vipaumbele vya matumizi kwa Wizara na Taasisi zake kama ifuatavyo:-

- i) **Kuimarisha upatikanaji wa elimu bora katika ngazi ya elimu ya lazima,** Wizara itajenga jumla ya madarasa 1,600 ya maandalizi, msingi na sekondari. Madarasa hayo yanajumuisha skuli 20 za kisasa za maandalizi, skuli tano za ghorofa za msingi, 10 za ghorofa za sekondari, skuli mbili za sekondari za wasichana, skuli tano za sekondari za amali, ujenzi wa mdarasa mpya pamoja na ukamilishaji wa madarasa yalioanzishwa na wananchi. Vilevile, Wizara itafanya ukarabati wa madarasa chakavu, kujenga vyoo 800 na sehemu za kunawia mikono kwa skuli za maandalizi na msingi na sekondari.
- ii) **Kuimarisha ubora wa ufundishaji na ujifunzaji,** Wizara itasambaza vifaa vya kufundishia na kujifunzia katika skuli zote, kutayarisha na kuchapisha vitabu vya mtaala mpya kwa madarasa ya kidato cha tatu, nne na sita, pamoja na kununua vitabu vya maktaba. Aidha, walimu

watajengewa uwezo juu ya matumizi ya mtaala mpya kwa kidato cha tatu, nne na sita, na vifaa vya utekelezaji wa mtaala rekebifu kwa wanafunzi wenye mahitaji maalum vitaandaliwa. Vilevile, mfumo wa tathmini ya kitaifa utanzishwa na tathmini kufanyika katika Darasa la Pili, Darasa la Tatu na Kidato cha Pili. Katika kuendeleza ujifunzaji wa kina, huduma za maktaba mtandao na Hifadhi ya Taifa ya Taarifa zitaanzishwa, gari la Maktaba-Tembezi litanunuliwa, na viwanja vya kisasa vya michezo katika skuli zenye michepuo ya michezo vitajengwa Unguja na Pemba pamoja na kuzipatia skuli vifaa vya michezo.

iii) **Kutanua na kuimarisha elimu ya Mafunzo ya Amali na Ufundi kwa kuzingatia soko la ajira**, Wizara itajenga skuli mbili za ufundi, karakana 1 kwa kila wilaya kwa ajili ya mafunzo ya amali na ufundi kwa wanafunzi wa sekondari, na kuanza ujenzi wa skuli tano za mafunzo ya amali. Vilevile, skuli za mafunzo ya amali zitapatiwa vifaa ili kuimarisha utoaji wa mafunzo hayo. Aidha, Wizara itajenga jengo la ofisi ya Mamlaka ya Mafunzo ya Amali pamoja na kujenga vyuo viwili vya mafunzo ya Amali, Bweleo na Chambani sambamba na ununuzi wa samani, vifaa vya mafunzo ya amali. Karakana za kufundishia na kujifunzia pia zitaimarishwa kwa kuzipatia vifaa na mashine za kisasa.

iv) **Kuimarisha matumizi ya TEHAMA na mifumo ya Kidijitali**, Wizara itasambaza vifaa vya TEHAMA kwa ajili ya kufundishia na kujifunzia katika skuli na kuunganisha skuli za msingi na sekondari na mkonga wa Taifa. Hatua

hii inalenga kuongeza matumizi ya teknolojia katika ujifunzaji, ufundishaji na usimamizi wa elimu, sambamba na kuimarisha upatikanaji wa huduma za kidijitali katika sekta.

- v) **Kuimarisha upatikanaji wa fursa za elimu ya juu,** Wizara itatanua miundombinu ya Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA) kwa kuendelea na ujenzi wa dakhalia za wanafunzi wa kike na kiume, ujenzi wa Chuo cha Ubaharia pamoja na miundombinu ya elimu katika Kampasi ya Tunguu ikiwemo jengo jipya la utawala, jengo la Skuli ya Elimu na Lugha, Kituo cha Huduma kwa Wanafunzi, nyumba nne za wafanyakazi na viwanja vya michezo. Aidha, Wizara itaiimarisha Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Karume (KIST) kwa kujenga hostel ya wanawake pamoja na tawi la Pemba na kuendelea na ujenzi wa ukumbi wa Taasisi hiyo. Aidha, Chuo cha Teknolojia cha India (IIT Madras) kitatanuliwa kwa awamu ya pili itakayojumuisha majengo ya utawala, madarasa, maabara, nyumba za walimu na migahawa. Sambamba na hatua hizo, idadi ya wanufaika wa mikopo ya elimu ya juu itaongezwa.
- vi) **Kuimarisha usimamizi na uongozi wa sekta ya elimu,** Wizara itajenga ofisi mbili za elimu na ukaguzi za mikoza, kuendelea na ujenzi wa jengo la ofisi Unguja, kukamilisha jengo la Wizara Ofisi ya Pemba na kununua samani za ofisi. Aidha, ukarabati wa jengo la ofisi Unguja utafanyika, pamoja na ujenzi wa ghala la Wizara Unguja. Vilevile, nyumba za walimu zitajengwa ili kuboresha mazingira ya kazi na huduma kwa walimu, sambamba na

ununuzi wa viti na meza za skuli kwa ajili ya kuimarisha mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji.

- 47. Mheshimiwa Spika,** Sasa naomba kuwasilisha mpango wa Utekelezaji wa maendeleo ya elimu kwa mwaka wa fedha 2026/2027 kwa mfumo wa programu kama ifuatavyo: -
- 48. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2026/2027, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali itaendelea kutekeleza malengo yake yaliyozingatia malengo ya Dira ya Maendeleo ya Taifa (2050), Ilani ya Chama cha Mapinduzi, Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDG), Mpango wa Mageuzi ya Sekta ya Elimu Zanzibar 2023 – 2030 (ZESTP), Ahadi za Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dkt. Hussein Ali Mwinyi pamoja na mikakati mengine ya kitaifa na kimataifa yenye lengo la kuimarisha upatikanaji wa huduma bora ya elimu nchini. Wizara pia, itaendelea kushirikiana na sekta nyengine zinazotoa huduma za jamii na kuimarisha uchumi ikiwemo Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango, Wizara ya Afya, Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi, Wizara ya Maji na Nishati na Madini, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara maalumu za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Aidha Wizara itaendeleza mashirikiano na washirika wa maendeleo wa ndani na nje na mashirika yasiyo ya kiserikali na wananchi kwa ujumla katika utekelezaji wa mpango wake kupitia programu sita na miradi mbalimbali ya maendeleo ya elimu.

- 49. Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka wa fedha 2026/2027, Wizara itatekeleza miradi mitatu ya maendeleo ambayo ni:-
- i. Mradi wa Uimarishaji wa Miundombinu ya elimu
 - ii. Mradi wa Uimarishaji wa Ubora wa Elimu
 - iii. Mradi wa Uimarishaji wa Elimu ya Juu.

MPANGO WA UTEKELEZAJI KWA MWAKA 2026/2027 KATIKA MFUMO WA PROGRAMU

- 50. Mheshimiwa Spika**, ufuatao ni mpango wa utekelezaji unaojumuishia madhumuni, utekelezaji wa shabaha, viashiria na shabaha za utekelezaji kwa kila programu.

PROGRAMU YA KWANZA: ELIMU YA MAANDALIZI NA MSINGI

- 51. Mheshimiwa Spika**, Programu hii ina madhumuni ya kumuandaa mtoto kimwili na kiakili kwa ajili ya kupata elimu ya maandalizi na msingi na kumuwezesha kujua kusoma, kuandika na kuhesabu na kumtayarisha kwa elimu ya Sekondari. Jumla ya **TSh. 261,795,159,428** zimepangwa kwa ajili ya kufanikisha kazi za programu hii. Kati ya fedha hizo, **TSh. 143,766,537,993** ni kwa matumizi mengineyo na **TSh. 118,028,621,435** kwa kazi za maendeleo.

Matokeo ya Muda Mfupi

- Wanafunzi waweze kujua kusoma, kuandika na kuhesabu.

Viashiria vya matokeo

- Asilimia ya uandikishaji.
- Uwiano wa walimu kwa wanafunzi.
- Uwiano wa wanafunzi kwa darasa.
- Asilimia ya Skuli zinazoendeshwa kwa mtindo wa zamu (shifti) moja
- Asilimia ya Ufaulu wa Mtihani wa Taifa wa Darasa la Saba.

Shabaha ya Utekelezaji

- Kuongeza kiwango cha uandikishaji wanafunzi wa maandalizi kutoka asilimia 81.6 kwa mwaka 2026 hadi kufikia asilimia 86.5 mwaka 2027.
- Kuendelea kuimarisha kiwango cha uandikishaji wanafunzi wa msingi kwa asilimia 100.
- Kupungua kwa uwiano wa wanafunzi kwa mwalimu kwa ngazi ya maandalizi kutoka 27 mwaka 2026 hadi 25 mwaka 2027.
- Kupungua kwa uwiano wa wanafunzi kwa mwalimu ngazi ya msingi kutoka 39 Mwaka 2026 hadi 37 mwaka 2027.
- Kupungua kwa Uwiano wa wanafunzi kwa darasa ngazi ya maandalizi kutoka 55 mwaka 2026 hadi kufikia 50 mwaka 2027.
- Kupungua kwa Uwiano wa wanafunzi kwa darasa ngazi ya msingi kutoka 64 mwaka 2026 hadi kufikia 60 mwaka 2027.
- Kuongeza asilimia ya Skuli zinazoendeshwa kwa mtindo wa zamu (shifti) moja kwa ngazi ya msingi kutoka asilimia 77.2 kwa mwaka 2026 hadi kufikia asilimia 80.0 kwa mwaka 2027.
- Kuongeza kiwango cha Ufaulu wa Mtihani wa Darasa la

saba kutoka asilimia 96.9 mwaka 2025 hadi kufikia asilimia 98.0 mwaka 2026.

PROGRAMU YA PILI: ELIMU YA SEKONDARI

52. Mheshimiwa Spika, Programu ya Elimu ya Sekondari madhumuni yake makubwa ni kumtayarisha mwanafunzi aweze kuendelea na masomo katika ngazi za juu zaidi. Jumla ya **Tsh. 361,355,005,925** zimepangwa kwa ajili ya kufanikisha kazi za programu hii. Kati ya fedha hizo, **Tsh. 136,621,235,925** ni kwa matumizi mengineyo na **Tsh. 224,733,770,000** kwa kazi za maendeleo.

Matokeo ya Muda Mfupi

- Kutoa elimu ya Sekondari
- kuongeza kiwango cha ufaulu wa wanafunzi.

Viashiria vya matokeo

- Asilimia ya uandikishaji
- Asilimia ya ufaulu wa wanafunzi katika ngazi ya Kidato cha Nne na Sita.
- Uwiano wa wanafunzi kwa mwalimu.
- Uwiano wa wanafunzi kwa darasa.
- Asilimia ya Skuli zinazoendeshwa kwa mtindo wa shifti moja.
- Asilimia ya wanafunzi wanaojiunga na elimu ya juu.

Shabaha za utekelezaji

- Kuongezeka kiwango cha uandikishaji wanafunzi wa Sekondari ya awali (Kidato cha 1 – 4) kutoka asilimia 80.2 kwa mwaka 2026 hadi kufikia asilimia 85.3 mwaka 2027.

- Kupungua kwa uwiano wa wanafunzi kwa darasa kutoka 50 mwaka 2026 hadi 45 mwaka mwaka 2027.
- Kuongeza asilimia ya Skuli zinazoendeshwa kwa mtindo wa zamu (shifti) moja kwa ngazi ya sekondari kutoka asilimia 83.2 kwa mwaka 2026 hadi kufikia asilimia 85.0 kwa mwaka 2027.
- Kuongeza kiwango cha ufaulu wa wanafunzi wa kidato cha nne kutoka asilimia 90.4 mwaka 2025 hadi kufikia asilimia 94 ifikapo mwaka 2027.
- Kuongeza kiwango cha ufaulu wa Wanafunzi wa kidato cha Sita kutoka asilimia 99.8 mwaka 2025 hadi kufikia asilimia 100 mwaka 2026.
- Kuongeza asilimia ya wanafunzi wanaojiunga na elimu ya juu.

PROGRAMU YA TATU: ELIMU YA JUU

53. Mheshimiwa Spika, programu hii madhumuni yake ni kutoa elimu itakayomuwezesha muhitimu kujiajiri au kuajiriwa. Jumla ya **Tsh. 220,223,294,615** zimepangwa kwa ajili ya kufanikisha kazi za programu hii. Kati ya fedha hizo, **Tsh. 37,997,751,115** ni kwa matumizi mengineyo na **Tsh.182,075,543,500** kwa kazi za maendeleo. Programu hii ina programu ndogo moja na maeneo matano ya huduma ambayo ni: -

Programu ndogo ya Mafunzo ya Ualimu

54. Mheshimiwa Spika, programu hii ina madhumuni ya kuwawezesha walimu kuwa wabunifu, wataalamu na wenye uwezo wa kuongoza ili kukuza ubora wa elimu.

Matokeo ya Muda Mfupi

- Uwepo wa walimu wenye umahiri watakaokuza ubora wa elimu.

Viashiria vya matokeo

- Idadi ya Wanafunzi waliojiunga na vyuo vya ualimu.
- Idadi ya walimu waliopatiwa mafunzo kazini
- Idadi ya walimu waajiriwa wapya waliopatiwa mafunzo.

Shabaha za Utekelezaji

- Kuongeza idadi ya wanafunzi wanaojiunga na vyuo vya ualimu kutoka 163 mwaka 2025 hadi kufikia wanafunzi 200 mwaka 2026.
- Kuongeza idadi ya walimu waliopatiwa mafunzo kazini kutoka 1,837 mwaka 2025 hadi kufikia 2,000 mwaka 2026.
- Kuongeza idadi ya walimu waajiriwa wapya waliopatiwa mafunzo kutoka 420 mwaka 2025 hadi kufikia 600 kwa mwaka 2026.

Huduma ya Elimu ya Juu, Ushauri na Utafiti

55. Mheshimiwa Spika, Huduma hii ina madhumuni ya kumtayarisha mwanafunzi kuingia katika fani za kitaalamu na ajira.

Matokeo ya Muda Mfupi

- Ongezeko la wahitimu wa kiwango cha elimu ya Stashahada, Shahada ya kwanza, Shahada ya pili na Shahada ya tatu katika fani mbali mbali za kitaalamu zinazohitajika katika maendeleo ya nchi.

Viashiria vya matokeo

- Idadi ya wahitimu
- Idadi ya programu mpya zinazoanzishwa
- Idadi ya tafiti zilizofanyika
- Idadi ya wanafunzi wanaojiunga na chuo.

Shabaha za Utekelezaji

